Makala hii imechunguza jinsi utandawazi unavyoakisiwa katika riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (2002). Imefanya hivyo kwa kuwa riwaya ya Kiswahili ni miongoni mwa tanzu zinazohakiki hali na harakati za utandawazi kwa mawanda mapana katika jamii za Kiafrika. Nadharia ya Usosholojia imetumika katika uhakiki wa taarifa

zilizowakilishwa. Mojawapo ya misingi yake ni kuichukulia fasihi kuwa ni kitengo pekee kilicho na uwezo wa kuakisi sayansi na utamaduni wa jamii unaodhibitiwa na miundo ya kijamii (Wamitila, 2002). Makala hii iliichunguza jamii kuwa ni malighafi ya fasihi. Mwandishi wa riwaya teule aliwekwa katika muktadha wake uliowazi ili kujua mwenendo na shughuli zake kwa kuwa kazi yake ni kiungo chake. Jamii iliyoandikiwa iliwekwa katika ulimwengu wake wa kawaida ili kufanya uhakiki wa kina. Nadharia hii imetumika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi na jamii kwa kurejelea riwaya za teule.

Utandawazi katika Riwaya Teule

Riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* (2002) iliandikwa kipindi ambacho mataifa ya Kiafrika yalianza kushuhudia maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia katika mifumo ya mawasiliano, sera za uchumi huria na mwingiliano mkubwa wa tamaduni, harakati zinazoongozwa na mataifa ya kibepali ya Ulaya na Marekani. Kwa kiasi kikubwa, kwa upande wa fasihi, maendeleo hayo yamebadili mkondo wa uandishi wa kazi zake kutokana na masuala yanayojidhihirisha katika mataifa ya ulimwengu wa tatu. Riwaya hii inachunguza na kurejelea nyuma nyakati za historia zilizopita za mataifa yanayoendelea barani Afrika na kuweka wazi matatizo yanayozikabiri baada ya Ukoloni katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Makala hii inaweka wazi hali ya utandawazi na uwekezaji unavyoyaathiri mataifa ya dunia ya tatu.

Utandawazi na Rushwa

Rushwa ni fedha au kitu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo (TUKI, 2004). Pia, hutumika kama njia za mkato bila kufuata taratibu zinazohusika kihalali. Katika riwaya teule, mwandishi amejadili kwa undani suala la rushwa linavyojitokeza katika jamii kwa namna mbalimbali. Rushwa inaakisiwa kupitia wawekezaji wa kigeni walioshamiri katika utoaji wa rushwa kwa vigogo wa serikali na vikaragosi vyao ili wawapigie debe (Chachage, 2009). Mmoja kati ya wawekezaji hao ni Mwingereza, Paul money aliyetoa rushwa kwa kuwarubuni vigogo na wananchi wanyonge wa delta ya mto Rufiji. Wajumbe wa Baraza la Mazingira kutoka Rufiji wanamwandama Lupocho. Mwandishi anaeleza:

> Kwanza wewe umeletwa na nani kwenye mkutano? Wewe na wenzako mlikuja hapa kutetea mradi ulioletwa na mwekezaji. Mmehongwa nyie (Chachage, 2002: 23).

Nukuu hii inaonesha namna baadhi ya wananchi wanavyoshirikiana na kuhongwa na wawekezaji ili kujinufaisha badala ya kuzingatia maslahi mapana ya umma. Kilichofanyika katika delta ya mto Rufiji kinafanyika pia katika nchi zetu za

ulimwengu wa tatu ambapo miradi mingi inayoanzishwa inakumbwa na hujuma kupitia mlango wa wawekezaji. Mataifa ya kibeberu yanafanya jitihada kubwa za kupambana na mataifa yanayoendelea ili kuhakikisha yanapora mali na rasilimali zake kwa kutumia mbinu mbalimbali. Vyombo vya uchumi vya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Dunia hutazamwa kama mawakala wa utandawazi unaondelea kuathiri mfumo na mitindo ya maisha na uchumi wa mataifa yanayoendelea (Sullivan, 1994). Pia, wapo viongozi wanaotoa rushwa ili kufanikisha mambo yao. Mwandishi anaaonesha suala hili kupitia mbunge aliyetoa rushwa kwa mkuu wa shule ya Ruhimba:

> Mkuu wa shule ya Ruhimba anadhihirisha kupokea rushwa na kudhubutu kusema mama mbunge wetu ametoa shilingi laki mbili leo asubuhi kwa ajili ya kutengeneza madawati ya shule ili watoto wetu wasome kwa raha (Chachage, 114).

Data hii inaonesha namna baadhi ya viongozi katika wanavyotoa na kupokea rushwa kwa maslahi yao mahsusi. Rushwa katika taasisi za umma ni miongoni mwa matatizo sugu yanayoathiri utoaji wa huduma zikiwemo za elimu, sheria na afya. Wakati mwingine, watu hukosa haki zao za msingi kutokana na baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kuwahudumia wananchi kukosa uzalendo katika utendaji na utekelezaji wa majukumu yao. Mkakati wa utandawazi uliasisiwa na kuimarishwa kupitia milango ya uwekezaji, ambapo mashirika ya umma, makampuni na taasisi za umma viliangukia mikokoni mwa wawekezaji (Mligo, 2015). Licha ya kuwa sera hii ililenga kukuza uchumi, baadhi ya viongozi waliokosa uzalendo kwa kuwa walishirikiana na wawekezaji kufaidi matunda yake kwa kiwango kikubwa.

Utandawazi na Dhuruma

Dhuruma ni kitendo cha kumnyima mtu haki yake. Dhuruma ni tendo lisilohaki, tendo la uonevu, ukatili na uovu dhidi ya haki za wanyonge (Ruhumbika, 1992). Dhuluma huweza kuzua migogoro, uasi na machafuko katika jamii. Pia, huweza kujenga na kuimarisha matabaka dhidi ya wadhulumaji na wale wanaodhulumiwa, wakiwemo wananchi wanyonge. Kuimarika kwa matabaka ni hatari kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii na taifa. Matabaka yanaweza kusigana katika harakati za msingi za kijamii na kitaifa. Dhuruma katika riwaya iliyochunguzwa yanaakisiwa kupitia kwa wahusika mbalimbali, hasa wanakijiji wa delta ya Rufiji, hasa katika kijiji cha Nyamisaki waliodhurumiwa kwa kukopwa nguvu zao na fedha baada ya kufanya kazi kwa uadilifu na uaminifu. Mwandishi anasema:

> Miaka ya sabini wananchi waliweza kununua mapande ya barafu kwa ajili ya kuhifadhi samaki wao bila matatizo. Mwanzoni mwa miaka ya themanini ndipo matatizo yalipoanza kutokea kiwanda kilipoanza kuwakopa wavuvi badala ya kuwalipa fedha taslimu

> na mabarafu yakaanza kukosekana, ingawa mabosi wa kiwanda waliendelea kunawiri zaidi (Chachage, 153).

Nukuu hii inaonesha namna miradi iliyoanzisha kwa malengo ya kuyasukuma maendeleo ya wananchi wazalendo, matatizo yalianza mara tu baada ya viwanda kubinafsishwa kwa kuanza kuwakopa wavuvi badala ya kuwalipa pesa taslimu. Matokeo yake wavuvi nao walianza kukosa fedha taslimu ili waweze kununua mabarafu na kuendelea na kazi ya kusindika samaki. Wananchi wanakopwa nguvu na jasho lao, nao wanaunganishwa kuwa wakopaji wa fedha taslimu katika kiwanda hicho hicho wanachokitumikia. Mtindo wa kukopwa unawaangukia wananchi, hasa wafanyakazi na wakulima wanaokopwa mazao yao yanayozalishwa kwa gharama kubwa kutokana na bei ya pembejeo kuwa ghari (Mligo, 2015). Hali hiyo imewatumbukiza wananchi katika hali ngumu ya maisha na umaskini mkubwa. Serikali haina budi kuzitazama upya sera za uwekezaji ili kuwanusuru na kuwasaidia wananchi.

Kwa hakika, yanayoelezwa katika riwaya teule yanaakisi hali halisi katika jamii katika kipindi hiki cha utandawazi na uwekezaji nchini Tanzania. Wananchi wameshuhudia kuwepo kwa madhira kadha wa kadha ambayo ni zao la uwekezaji hapa nchini. Mwandishi ameonesha namna mashirika ya fedha ya kimataifa yanavyowakopa wakulima ambapo mazao yao yameendelea kudhoofishwa kwa kutolipwa kwa wakati licha ya kupanda kwa pembejeo za kilimo na bei ya mazao kuwa chini. Mfumo wa uwekezaji wa kiuchumi usiojikita katika uchunguzi wa kina kuhusu faida na hasara zake umeua viwanda vya ndani vilivyokuwa vimestawi vizuri kabla ya kuimarika kwa sera za uwekezaji katika jamii za Kiafrika (Offiong, 2001). Wawekezaji wanashirikiana na viongozi wazawa kufanya sherehe zisizo na tija kwa wananchi na taifa lao. Mwandishi anasema:

> Kila kiongozi alipofika kijiji kililazimishwa kuandaa sherehe na chakula kwa madai kwamba utamaduni wa Mwafrika ni ukarimu kwa kila mgeni ajapo, ingawa viongozi hao walikuwa wakilipwa masurufu na serikali (Chachage, 87).

Maelezo hayo yanaonesha namna vijiji vinavyozunguka bonde la delta ya mto Rufiji vilivyodhulumiwa na kuhujumiwa kwa kunyang'anywa mashamba bila kulipwa fidia kama haki yao ya msingi ya kisheria na kiutendaji. Serikali yao iliungana na wawekezaji wa kibeberu kuvifuta baadhi ya vijiji kwa madai kuwa hawakupokea agizo la serikali kuhusu kilimo cha tumbaku. Wananchi waliporwa rasilimali na tabaka la juu la watu wachache kwa kupanga na kufanya matumizi makubwa kwa kuandaa bajeti za vikao na sherehe kwa misingi ya kuwakarimu viongozi wao (Katembo, 2005). Jamii haina budi kuitikia wito uliotolewa na Raisi wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyepinga na kupiga marufuku vikao

vya serikali kufanyika katika kumbi za mahoteli kwa gharama kubwa na wahusika hujilipa posho kubwa. Marufuku hiyo inalenga kupunguza matumizi ya serikali yasiyokuwa ya lazima.

Utandawazi na Uwekezaji

Siasa na uchumi ni vitu pacha ambavyo haviwezi kutengana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Siasa ndicho chombo muhimu kinachoundwa ili kutekeleza sera mbalimbali zinazohusu uchumi na maendeleo katika taifa linalohusika (Mbarouk, 2017). Mwandishi katika riwaya teule amezungumzia suala la ujenzi wa vijiji vya Ujamaa na Kujitegemea sera iliyoasisiwa na hayati Baba wa Taifa, Julius Kambarage Nyerere miaka ya 1960 na 1970 kupitia Azimio la Arusha. Mwalimu J. K. Nyerere alikusudia kujenga taifa lenye misingi ya ujamaa na kujitegemea ili kujenga uchumi imara wa taifa, ingawa sera hii ilionekana kupingwa na mataifa yaliyoendelea kwa maslahi yao ya kiuchumi. Mataifa yaliyokuwa yameimarika kuichumi yalifanya jitihada kubwa za kuudhoofisha mfumo huo ili kupenyeza maslahi yao katika mataifa yanayoendelea. Mfumo wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea unatazamwa kama ulianzishwa nchini Tanzania kabla ya kujengeka na kufungamana kikamilifu na mifumo wa Kibeberu. Mwandishi anaeleza:

> Nchi nyingine ambazo hazijaendelea kusubiri kwamba tatizo la Tanzania lilikuwa ni kupapukia mfumo wa Ujamaa mapema mno kwani kufuatana na mafunzo ya mwana falsafa Max, ilibidi Tanzania na ubepari ujikite vya kutosha kwa kuwasaidia mabepari wazalendo ndipo baada ya hapo Ujamaa ungewezekana kujengeka madhubuti (Chachage, 9I).

Maelezo hayo yanaeleza namna vita ya Ubeberu na Ukomunisti vilivyojengeka katika mataifa yanayoendelea. Kuanzishwa kwa mfumo wa siasa za Ujamaa na Kujitegemea kulizua mjadala uliolenga kuonesha mvutano baina ya baadhi ya wananchi waliowalaumu viongozi wao kuwa waliamua kuwaita wawekezaji bila kuwashirikisha wananchi wao ambao ndio wamiliki na walinzi wa rasilimali za taifa lao. Kwa wakati huo, tabaka la viongozi halikuamini kwamba bila wawekezaji maendeleo hayawezi kupatikana kirahisi (Chachage, 2003). Kinyume na matarajio yao, mradi wa uwekezaji wa ufugaji wa kamba uliishia kuharibu mazingira ya asili na kuteketeza misitu ambayo ilikuwa inatunzwa kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa. Wawekezaji waliamua kuanzisha miradi isiyo na tija kwa wananchi kwa kuzingatia mazingira yao. Serikali ilishirikiana na wawekezaji kuvifuta vijiji vilivyokuwa vikipinga kilimo cha tumbako kilichoonesha kama hakikuwa na maslahi ya moja kwa moja na wananchi na taifa lao. Mwandishi anaeleza:

> Serikari ilivyoviingilia vijiji hivi vilivyojitegemea na kuvivunja kwa kuonekana na kuwatishio kubwa kwa serikari, hasa baada ya wanavijiji hawa kukataa kulima zao la tumbaku wakidai kwamba kwao ilikuwa faida kubwa zaidi kulima mazao ya chakula. Hoja

> ya wananchi iliwaudhi wanasiasa na hasa mkuu wa mkoa Bwana Edward Barongo (Chachage, 107).

Data hii inaonesha namna mamlaka ya juu ya kisiasa inavyoweza kufanya maamuzi yasiyo na tija dhidi ya raia wake kwa kuwalazimishwa kutekekeleza matakwa yao. Wananchi wa bonde la mto Rufiji walilima mazao ya chakula ambayo walidai yalikuwa na faida kuliko tumbaku kwa kuzingatia mazingira yao. Mkuu wa mkoa alilazimika kuwalazimisha wanancha ili kuwaridhisha wawekezaji wa kigeni. Serikari ililazimika kuviingilia vijiji vya wananchi na kuvivunja. Mwandishi anaonesha jinsi wawekezaji wanavyovuruga misingi ya uzalishaji wa kiasili katika baadhi ya mataifa ya Kiafrika. Pia, anaonesha namna jitihada zinazofanywa na baadhi ya viongozi wazawa wasivyotetea rasilimali zilizopo na wananchi kwa kufungamana na wawekezaji kwa manufaa yao. Kama ilivyokwishaelezwa, mwandishi anaonesha namna wananchi wa bonde la mto Rufiji walivyosimama kidete kutetea rasilimali za taifa lao, ingawa hawakupata msaada wowote kutoka serikalini. Hivyo, ndivyo wawekezaji wa kigeni walivyo na nguvu zaidi kuliko wazawa na serikali zao. Sheria za nchi zipo, lakini zimenyamazishwa kwa makusudi kwa maslahi nyeti ya vikundi vya watu wachache, hasa baadhi ya viongozi na wawekezaji wenye uchu na tamaa ya kujinufaisha.

Uwekezaji katika mataifa ya Kiafrika unafanywa bila kuzingatia maslahi ya wananchi na taifa. Hakuna faida yoyote ya wazi inayopatikana katika uwekezaji kulingana na udhaifu wa mikataba inayosainiwa na viongozi wasio waadilifu katika wa mataifa yanayoendelea. Mara nyingi mataifa hayo yameishia kupata faida kidogo na wananchi wake kuangukia katika mfumo unaowanyanyaswa na kuwadhalilishwa. Kuhusu mfumo wa soko huria unaoendelea kuimarika, pamoja na utoaji wa misaada ya mikopo kutoka katika mataifa ya kibepari, mwandishi ameonesha jinsi inavyozidi kuathiri uchumi wa mataifa ya ulimwengu wa tatu. Kwa hakika, lengo lao si kuyanufaisha mataifa yanayoendelea, bali wanakusudia kuyafanya mataifa hayo kuwa vitalu na vitega uchumi vya uwekezaji vinavyoyafanya mataifa yanayoendelea kuwa tegemezi kuichumi, kisayansi na kiteknolojia (Simala, 2003). Kwa bahati mbaya, uwekezaji wao una mchango mkubwa katika kudhoofisha na kuua viwanda vya ndani; na viongozi wamekosa ujasiri na nguvu ya kukemea jitihada na hujuma za kibepari.

Utandawazi na Uongozi

Suala la uongozi limejadiliwa kwa kirefu katika riwaya teule. Viongozi wamechorwa katika sura mbalimbali zinazoonesha hali halisi kulingana na namna wanavyojipambanua kwa kuwa wengi wao wamejaa usaliti, ubinafsi, uchu wa madaraka na kutaka kutawala daima. Baadhi yao hawafanyi tathmini kuhusu ubora na udhaifu wao katika kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya mataifa

wanayoyaongoza. Pia, wengi hupenda anasa, kuabudiwa, wamejaa majivuno, dharau, hawajiamaini na baadhi yao ni vibaraka wanaotumiwa na mabepari kunyonya uchumi wa mataifa yao (Ryanga, 2002). Kwa mfano, Kwa kurejelea wananchi wa kijiji cha Nyamisati, uongozi mbaya wa bwana Lupocho umeonesha uroho wa kupenda pesa na kujinufaisha kwa maslahi yake binafsi. Hali hiyo ilikuwa tofauti na bwana Nyamilanzi aliyechorwa kama kiongozi bora aliyewashirikisha wananchi wake kikamilifu katika usimamizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Nyakirama anasikika akilalama kuhusu uongozi mbaya:

> Walikuwa wamefikiwa na ugeni wa Makamu wa Raisi asubuhi. Hivyo, wanataka kufuga kamba. Tunasikia kama wanataka kuchimba handaki Rufiji yote na kutuhamisha tukaishi kwingine (Chachage, 152).

Maelezo haya yanaonesha namna wanachi wasivyopewa nafasi ya kushirikishwakatika mipango ya maendeleo ya miradi inayoanzishwa katika katika maeneo wanayoishi. Pia, inaonesha namna wananchi wa delta ya mto Rufiji walivyopelekewa mradi wa kufuga kamba bila kushirikishwa wananchi kwani maoni na matakwa ya wawekezaji ndiyo yanayopewa kipaumbele. Kitendo cha wananchi kutoshirikishwa katika mipango na maamuzi kilileta mgogoro kati ya wawekezaji na wananchi wa bonde la mto Rufiji. Jambo hilo linazua migogoro isiyokuwa ya lazima baina ya wananchi na wawekezaji katika mataifa mengi. Suala la kutowashirikisha wananchi katika miradi inayofanyika katika sehemu wanazoishi kinaleta migogoro kwa wananchi kiasi cha kuleta athari katika utekelezaji wa miradi inayohusika (Amatubi, 2002). Pia, kuna baadhi ya viongozi wazawa wenye kauli mbaya zinazowakatisha tamaa wananchi na kuchochea chuki kwani wanatoa hotuba zenye utata unaozua mijadala ya kuhitilafiana nao. Kwa mfano, Waziri Mkuu alipozuru na kuhutubia wananchi wa kijiji cha Nyamisati, hotuba yake iliwagawa wanakijiji. Mmoja wa wanakijiji kwa masikitiko alisikika akilalama juu ya hotuba ya Waziri Mkuu:

> Haikuwa hotuba, bali yalikuwa matusi kwa kadri tunavyofahamu sisi. Alidai kwamba sisi watu wa Rufiji ni wavivu ndivyo maana hatuna maendeleo. Alidai kwamba rasilimali tunazo, lakini tumezikalia na kutokana na tabia zetu za kishirikina, sasa tuna pinga uwezekano wa kuwepo kwa mradi wenye tija kwa maslahi ya wananchi na taifa (Chachage, 114).

Data hii inafafanua athari na tabia za viongozi kutowashirikisha wananchi katika mipango ya maendeleo namna inavyozua mgogoro. Pia, inaonesha matumizi mabaya ya jukwaa kwa baadhi ya viongozi wanavyojali maslahi ya wawekezaji bila kufuata

kanuni, sheria za nchi na misingi ya utawala bora na katiba wa taifa linalohusika. Viongozi wengi wanashindwa katika uteuzi mzuri wa lugha na maneno ya busara ili kuepusha migongano ya kimaslahi isiyokuwa ya lazima (Bhalla, 2006). Riwaya hii imeweka wazi namna wazalendo waliopigania uhuru katika mataifa ya Kiafrika walivvyosahauliwa baada ya uhuru kupatikana kwani wengi wa viongozi waliopo sasa wanawapa fursa pana wawekezaji wa kimataifa, wale wale waliokuwa wametutawala. Mwandishi anasema:

> Watu wengi waliopigania uhuru walisahaulika, Robert Makange na wenzake, akiwemo Kheri Rashid Bhangdellah walipata misukosuko hata kufungwa kwa sababu ya gazeti lao la Mwafrika. Pia, kusahauliwa kwao kulitokana na wingu la uuzaji wa uhuru uliopiganiwa na vipande vya ardhi pasipo kificho kuanzia huko Loliondo hadi Rufiji vilikuwa vikiuzwa kwa watu wale wale waliong'olewa miaka ya sitini, kisha wananchi waliambiwa na Makamu wa Raisi kuwa hawapendi maendeleo kwa sababu walikuwa wanapinga kuuza ardhi kwa kung'olewa; na haya ndiyo yametufikisha Waafrika wengi hapa kwenye matatizo (Chachage, 213).

Rekodi hii inafafanua namna wananchi wazawa walivyojitoa kwa moyo wa uzalendo kupambana kwa masilahi ya taifa wanavyopuuzwa mara baada ya utumishi wao kukoma. Baadhi ya viongozi wa Kiafrika wamesahau lengo la kuimarisha uchumi na misingi ya maendeleo ya mataifa yao kwa kufuata katiba, utawala wa haki na sheria. Wengi wao wamekuwa vinara wa kusababisha migogoro katika mataifa wanayoyaongoza na wakati wote wamekuwa katika wingu zito la kuwa mawakala wa wawekezaji wa kigeni, huku wakipuuzia matatizo ya wananchi na harakati zao za kupigania maendeleo ya nchi kwa kuendelea kuuza ardhi bila kufanya tathmini ya kutosha kuhusu faida na hasara zake.

Viongozi hawana budi kuwa makini katika kuupokea na kuuendeleza uwekezaji wa kigeni kwa maslahi mapana ya wananchi na taifa lao. Aidha, wanaaswa kutoupokea mfumo wa soko huria kwa pupa bila kuchuja ili kubaini maslahi mapana yenye tija kwa taifa. Mataifa ya kigeni hutumia mbinu nyingi ili kufanikisha madhumuni yao ya kunyonya uchumi wa mataifa yanayoendelea kwa mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kutoa misaada ya huduma za jamii kibiashara, kijeshi, kiteknolojia, taasisi za kifedha, likiwamo shirika la Fedha la Dunia na Benki ya Dunia. Mataifa hayo hulazimika kutoka nje ya mipaka yao ili kujiimarisha kijiografia, kimasoko na kimalighafi (Little, 1996). Pia, hutumia mbinu za utengenezaji wa viongozi vibaraka wanaosimamia utekelezaji wa sera zao za kiuchumi kwa maslahi yao.

Demokrasia na Utandawazi

Suala la demokrasia na mifumo mbalimbali ya maamuzi ya kisiasa katika jamii nyingi za Kiafrika limejadiliwa kwa namna mbalimbali. Baadhi ya wanasiasa wanashikamana na kushirikiana kikamilifu na mabeberu kupuuza nguvu ya ushirikishwaji wa wananchi katika kutoa mamuuzi sahihi kwa manufaa ya umma (Mayega, 2006). Katika riwaya teule, viongozi wa delta ya Rufiji waliitisha uongozi mkubwa ili kumnadi mwekezaji wa kamba kutoka nchini Uingereza. Viongozi wenye mamlaka ya juu kitaifa na kisiasa walifanya maamuzi na ushawishi mkubwa kupenyeza matakwa yao bila kuwashirikisha wananchi wao. Katika kudhihirisha haya, mwandishi anaeleza:

> Mkutano uliitishwa na viongozi wa Baraza la Mazingira na kufanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Utamaduni wa Korea kuhusu mapendekezo ya mwekezaji kutoka Uingereza, bwana Paul Mooney, ambaye alitaka kuanzisha ufugaji wa kamba katika delta ya Rufiji. Yalikuwepo mashirika ya nchi za wafadhili na jumuiya zisizo za kiserikali bila kuwashirikisha wanarufiji katika mkutano wa kujadili uwekezaji wa Mwingereza (Chachage, 22).

Maelezo haya yanaonesha namna nguvu ya mamlaka na madaraka ya kisiasa nchini ilivyo na nguvu ya kufanya mamuuzi yanayopuuza haki na demokrasia. Miradi mingi inaanzishwa bila kushirikisha wataalamu wazawa waliopo nchini ili kutoa maoni kulingana na mazingira yao, lakini nafasi zao zinachukuliwa na viongozi wanaohodhi madaraka. Viongozi waliitisha kikao bila kushirikisha na kuheshimu mawazo ya wananchi wanaowaongoza. Ili kuimarisha uhai na mshikamano baina ya viongozi na wananchi inapaswa viongozi kuwashirikisha kikamilifu wananchi wao wakati wa kufanya maamuzi, hasa matumizi ya rasilimali za umma ili kudumisha amani na utulivu nchini. Amani na utulivu tunu za taifa; na ni ngao na nguzo muhimu katika ujenzi wa jamii endelevu (Njihia, 2005). Pamoja na dhamana waliopewa ya kuongoza wengine, bado kuna masuala ambayo yanahitaji ushirikishwaji wa umma katika vikao muhimu vya maamuzi. Kupuuza demokrasia kunaweza kusababisha uvunjivu wa amani pamoja na kuleta hali ya kutoelewana kati ya viongozi na wananchi wao.

Hitimisho

Kuimarika kwa mfumo wa utandawazi na sera za soko huria katika jamii za Tanzania na kwingineko barani Afrika, wananchi wameshuhudia kasi ya kudhoofika kwa uchumi, uharibifu wa mazingira na rasilimali za umma, ukosefu wa haki na usawa, dhuluma na misukosuko mikubwa inayozigharimu jamii nyingi katika mataifa yanayohusika. Kwa kurejelea riwaya teule ya *Makuadi wa Soko Huria*, kwa kiasi kikubwa, mwandishi ameonesha hali halisi iliyoakisiwa katika jamii nyingi za Afrika

Mashariki na kwingineko barani Afrika. Miongoni mwa masuala hayo yanahusu athari za sera za utandawazi na uwekezaji kama zilivyodokezwa katika makala hii. Kwa kawaida, matatizo hayo yanaathiri kila fani ya maendeleo ya jamii na taifa. Wajibu wa jamii na mataifa ya Kiafrika ni kujenga misingi imara itakayoyawezesha mataifa yanayohusika kujitegemea katika nyanja zote za kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi; pamoja na kulinda tunu na amali za taifa kwa manufaa ya taifa na wananchi wake. Mataifa ya Kiafrika hayana budi kujikosoa na kujisahihisha ili kuzifanyia marekebisho sera za utandawazi ili ziwe na tija kwa maslahi mapana ya taifa na wananchi wake.

Marejeleo

Amatubi, M. N. (2002). 'Globalization and Mainstreaming of Kiswahili Research in the 21StCentuary', katika Utafiti wa Kiswahili. Maseno: Chuo Kikuu cha Maseno, uk. 43 – 48.

Chachage, S. C. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*. DUP: Dar es Salaam.

Chachage, S. C. (2003). *Kiswahili katika Muktadha wa Utandawazi*. BAKITA

Chachage, C. S. L. (2009). 'Ndani ya Bongo, Utandawazi na Mgogoro wa Utamaduni'. Imepakuliwa http:/www.redet.udsm.ac.tz (08. 01. 2020).

Jauch, H. (2001). *Playing the Globalisation Game: The Implications of Economic Liberalisation for Namibia.* Windhoek: Labour Resource and Research Institute (LaRRI).

Katembo, I. B. (2005). Kiswahili, the Global Economy and the African American. Seminar Paper Presented at the International Symposium on Kiswahili Language and Globalization. Tanzania, University of Tanzania.

Khamis, S. A. M. (2007). 'Utandawazi au Utandawizi? Jinsi Lugha ya Riwaya Mpya ya Kiswahili Inavyodai' katika *Kiswahili*, Juzuu Namba 70. Dar es Salaam: TUKI. Kur, 47 - 66.

Khayesi, M. K. (2000). 'Kiswahili and Information Technology (I. T): Challenges in Public University Libraries in Kenya' katika Kiswahili Juzuu 65. TUKI, uk. 24 – 28.

Little, A. (1996). Grobalization and Education Research: Whose Context Counts? International Journal of Development, Vol. 16, No. 4. OK. 427 – 438.

Mayega, P. (2006). *Mwalimu Mkuu wa Watu*. Dar: MBP Interprises.

Mbarouk, S. S. (2017). *Usasabaadaye Katika Riwaya ya Walenisi.* Katika Jarida la Sumait University Journal, Na.3, uk.1-16.

Mligo, E. S. (2015). *Utandawazi katika Mazingira ya Kanisa la Tanzania* (Hakijachapishwa). Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Mwangosi, G. (2016). 'Utandawazi wa Kiswahili: Mitazamo ya Ukubalifu na Mkwamo kama Lugha Rasmi ya Afrika', *Ruaha Journal of Social Sciences (RUJASS),* VOL, 2: 41 - 50.

Nicol, B. (2002). *Postmodernism and the Contemporary Novel, A Reader*. Edinburg Univesity Press.

Njihia, S. K. (2005). *Kiswahili na Utandawazi, katika Insha za Jubilei 2005, Utandawazi na Umoja wa Afrika*. TUKI.

Offiong, D. (2001). *Globalisation: Post-Neodependency and Poverty in A frica*. Enugu Nigeria: Fourth Dimension Publishing Co.

Ruhumbika, G. (1995). *Miradi Bubu Ya Wazalendo.* Dar es salaam: Tanzania Publishing House Limited.

Ryanga, S. (2002).'The African Union in the Wake of Globalization: The Forgetten Language Dimension' katika *Kiswahili Juzuu 65*. Dar es Salaam: TUKI, UK. 1-15.

Sarup, M. (1989). *An Introduction Guide to Poststructuralism and Postmodernism*. Athens: University of Georgia Press.

Sweeting, A. (1996). The Grobalization of Learning: Paradigm or Paradox? International Journal of Development Vol. 16, No. 4 uk. 379 – 391.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi*. Mombasa: Phoenix Publishers Limited.

Mtazamo wa Jamii ya Kiganda Kuhusu Kiswahili: Uchunguzi wa Wajifunzaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere

Arnold, B. G. Msigwa
Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
agawasike@gmail.com

Ikisiri

Makala hii inachunguza sababu za wanafunzi wachache kuchagua kujifunza lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Uchunguzi umefanywa kutokana na tangazo lililotolewa na serikali ya Uganda kuwa ifikapo mwaka 2020 lugha ya Kiswahili itakuwa somo la lazima katika shule za msingi na sekondari nchini humo. Data za utafiti huu zilikusanywa uwandani kwa njia ya mahojiano na walimu wanaofundisha Kiswahili kwa ngazi ya shahada za awali na umahiri na wanafunzi wanaosoma Kiswahili Chuo Kikuu cha Makerere. Data zilikusanywa katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Watoa taarifa wakiwa ni wanafunzi wa shahada za awali na umahiri, pamoja na walimu wanaofundisha shahada za awali na umahiri. Uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Modeli ya Elimu Kijamii. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu kwa ngazi ya shahada za awali na umahiri ni wachache. Uchache huo unatokana na matumizi ya Kiswahili yamejenga katika mtazamo hasi kwa Waganda waliowengi kwa sababu kinatumika na wahalifu kwa madhumuni mbalimbali. Uchechefu huo umesababisha kushindikana kutekelezwa kwa sera ya serikali ya Kiswahili kuwa kama somo la lazima hadi ilipofika 2020.

Utangulizi

Binadamu yeyote aliyekamilika huishi katika muktadha wa kijamii na watu wenye tabia na mitazamo tofauti kuhusu mambo mbalimbali. Matukio na matendo yanayofanywa na watu hao wanaomzunguka binadamu huwa na athari ya moja kwa moja katika kuvichukulia vitu, ikiwa ni pamoja na lugha wanayotumia watu hao. Athari hizo zinaweza kuwa ni chanya au hasi kutegemea na mhusika alivyokabiliana nazo. Uamuzi wa kuamua kujifunza lugha kunaweza kuathiriwa na namna watu wanaomzunguka wanavyoitumia na wanavyoiona lugha inayohusika. Katika Chuo Kikuu cha Makerere idadi ya wanafunzi wanaochagua kusoma Kiswahili ni ndogo ikilinganishwa na mwelekeo wa serikali ya nchi hiyo ya kukitandawaza Kiswahili katika shule msingi na sekondari. Makala hii imechunguza sababu za uchechefu wa wanafunzi wanaochagua kusoma somo la Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda.

Usuli wa Utafiti

Uchunguzi umefanywa kutokana na tangazo lililotolewa na serikali ya Uganda kuwa ifikapo mwaka 2020 lugha ya Kiswahili itakuwa somo la lazima katika shule za msingi na sekondari nchini humo. Licha ya sera hiyo, mtafiti alibainika kuwapo kwa idadi ndogo sana ya wanafunzi wa shahada za Awali na Umahiri katika Chuo Kikuu cha Makerere wanaosoma Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi wa Umahiri mwaka wa kwanza alikuwa mwanafunzi 01 na mwaka wa pili walikuwa wanafunzi 02 tu. Kwa wanafunzi wa shahada za Awali, mwaka wa tatu walikuwa 40, mwaka wa pili 30 na mwaka wa kwanza 52 tu. Wakati idadi ya wanaojiunga kusoma lugha ya Kiswahili ikiwa ni ndogo, mahitaji ya walimu katika shule za sekondari zinazofundisha Kiswahili ni makubwa. Mathalani, mwanafunzi wa mwaka kwanza katika shahada ya Umahiri alibainika anafundisha shule tatu somo la Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita. Uchechefu wa wanafunzi wanaojiunga kusoma Kiswahili katika ngazi ya Chuo Kikuu nchini Uganda licha ya kuwapo kwa fursa za wazi za ajira kupitia Kiswahili ndiyo ilichochea kufanya utafiti huu ili kubainisha sababu za hali hiyo.

Lengo ya Utafiti

Lengo la jumla la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza sababu za kuwapo idadi ndogo sana ya wanafunzi wanaochagua kusoma lugha ya Kiswahili katika ngazi ya Chuo Kikuu nchini Uganda. Sampuli ya utafiti ilikuwa ni walimu wa Kiswahili kwa ngazi ya shahada ya Awali na Umahiri katika Chuo Kikuu cha Makerere na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katika shahada za Awali na Umahiri. Mahojiano ya wazi yalifanyika kati ya mtafiti na watoa taarifa ili kupata taarifa zilizokuwa zikichunguzwa. Swali muhimu lililojibiwa ni kwa nini idadi ya wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili ni wachache katika Chuo Kikuu cha Makerere? Data za mahojiano zilikusanywa kutoka kwa wanafunzi 02 wa Umahiri, wanafunzi 15 wa Shahada za Awali na walimu 02 wanaofundisha Kiswahili Chuo Kikuu cha Makerere. Pia, mwalimu 01 wa shule ya sekondari ambaye ni mwanafunzi wa umahiri chuoni hapo alihojiwa. mwalimu wa shule ya sekondari alishiriki ili kuthibitisha data zilizopatikana kutoka kwa watoa taarifa wa Chuo Kikuu cha Makerere.

Mapitio ya Maandiko

Ujifunzaji wa lugha ya pili (Lg2) ni mchakato unaomhitaji mjifunzaji lugha kuwa tayari kujifunza ili mjifunzaji aweze kupata misamiati ya kutosha itakayomwezesha kuwasiliana. Ikiwa Mjifunzaji ikiwa hatakuwa na motisha ya ndani wa kujifunza lugha, kuna uwezekano mdogo wa kumudu lugha anayojifunza (Brecht, 2000). Motisha ni kitu muhimu kwa mjifunzaji wa Lg2 ili kuweza kupata umilisi wa lugha anayojifunza. Motisha binafsi ni muhimu kwa kuwa ndiyo inayoukilia umilisi na uelewa wa kitu ajifunzacho mtu katika mazingira ya shule (Deci na Ryan, 1985).

Wanafafanua zaidi kwamba, wajifunzaji wawapo shuleni hutumia masaa mengi ya kuchangamana na wanajamii wengine. Mchangamano huo unarahisisha ujifunzaji wa lugha, Sykes (2015) anabainisha mambo matatu yanayoukilia umuduji wa Lg2. Mambo hayo ni motisha, muktadha na mtazamo kama yalivyodokezwa katika sehemu hii.

Motisha

Motisha ni tabia inayomsukuma mtu kutimiza malengo fulani. Motisha ni tuzo anayopewa mtu kumshajiisha kufanya jambo; kivutio (BAKIZA, 2010). Motisha ni ule msukumo unaomfanya mjifunzaji wa lugha ya kigeni ajifunze lugha fulani anayotaka kujifunza. Katika uelekeo huo, wafundishaji wa lugha ya kigeni wana jukumu la kuwamotisha wajifunzaji wa lugha kwa kutengeneza mazingira mazuri yatakayowafanya wajifunzaji kupenda kujifunza lugha wanayojifunza. Motisha za wajifunzaji wa lugha ya kigeni zimeainishwa kwa namna tofauti na wanaisimu tumizi kutegemea vigezo mbalimbali. Brown (2004) amegawa motisha katika makundi makuu mawili: Motisha ya ndani na motisha ya nje. Uainishaji huo ulizingatia ubadilifu wa mjifunzaji kutegemea na mazingira. Crookers na Schidt (1991) wanadai kuwa motisha inaweza kuainishwa kwa kuzingatia sababu za mjifunzaji kujifunza lugha nayohusika, utashi wa kutaka kufanikisha jambo na uelekeo wa mjifunzaji katika mazingira ya ujifunzaji lugha na jitihada za mjifunzaji.

Al-Bustan na Al-Bustan (2009) wanadai kuwa motisha inaweza kuwekwa katika makundi makuu sita. Makundi haya ni motisha kwa kuzingatia mwelekeo wa mjifunzaji kuhusu jamii, kujiamini kwa mjifunzaji na matarajio yake katika kufaulu na uwazi na uhalisi ili kufikia malengo.mengine yanahusu kushiriki; mjifunzaji kushiriki na kushirikishwa katika kujifunza lugha, muktadha, msaada wa mazingira anaoupata mjifunzaji, pamoja na sifa binafsi za mtu, kipaji, umri, jinsia na uwezo wa kumudu lugha. Wataalamu wengi wanaona kuwa motisha inaweza kugawika katika aina mbili, motisha ya juu na motisha ya chini. Motisha ya juu inaweza kutokea ikiwa mjifunzaji wa lugha atajichanganya na jamii ili kubadili uono wake kuhusu jamii hiyo kutaka kupata madaraka au hadhi. Motisha ya chini itatokea ikiwa hayo mambo yatakosekana kwa mjifunzaji wa lugha. Hivyo, kuna namna nyingi za kutazama motisha. Uelekeo unaochukuliwa katika kazi hii ni mgawanyo wa motisha kama ulivyofanywa na Sykes (2015).

Sykes anaeleza kuwa motisha katika ujifunzaji wa Lg2 inaweza kugawanywa katika makundi matatu. Kwanza, kuna motisha tumizi, mahitaji ya mawasiliano ya mjifunzaji. Hii ni aina ya motisha ambayo inahusishwa moja kwa moja na malengo ya kujifunza lugha. Cook (2013) anataja baadhi ya malengo ya watu kujifunza Lg2 kuwa, mtu anaweza kujifunza Lg2 au ya kigeni ili kufaulu mitihani au kupata aina fulani ya kazi. Katika muktadha wa ujifunzaji lugha za kigeni shuleni hili ndilo

linaweza kuwa lengo kuu. Kwa hivyo, wajifunzaji wanasukumwa kujifunza lugha ili tu waweze kutimiza malengo ya mtihani au kazi kuliko mahitaji ya kumudu na kuelewa lugha kwa azma ya kuweza kuwasiliana. Mjifunzaji wa lugha ya kigeni anayesukumwa na mitazamo ya nje, mtazamo wake kuhusu lugha unaweza kuwa hasi. Hivyo, uwezekano wa kumudu lugha inayohusika unakuwa mdogo. Mjifunzaji wa lugha ya Kiswahili ikiwa ni lugha ya kigeni anayesukumwa na mahitaji ya nje.

Pili, kuna motisha changamani na mtazamo wa mjifunzaji kuhusu lugha na utamaduni wa lugha lengwa inayohusiana na kiwango cha mjifunzaji lugha anavyojitambulisha na kujinasibisha na wazawa wa lugha na utamaduni wao wa lugha inayolengwa. Mjifunzaji lugha anajitanabaisha kwa upande chanya na wazawa wa lugha anayojifunza na kutumia lugha hiyo kwa mawanda mbalimbali hupata umilisi mzuri wa lugha anayojifunza. Mjifunzaji huyu anasukumwa na nia ya kujua lugha, utamaduni na wanalugha katika mazingira mbalimbali. Motisha changamani na mtazamo wa mjifunzaji lugha kuhusu utamaduni wa lugha lengwa hurejelea hali ya mjifunzaji Lg2 kutafuta weledi wa lugha anayojifunza na kutambua thamani ya kuwasiliana kwa kutumia lugha lengwa, akisukumwa na umilisi wa Lg2 (Lightbown na Sapada, 2006). Motisha changamani inapokuwa juu, mjifunzaji wa Lg2 hutafuta miktadha zaidi ya kufanyia mazoezi. Wakishadidia hoja hii ya motisha changamani na mjifunzaji wa Lg2 kutafuta mazingira zaidi ya kufanyia mazoezi, Gardner na Lambert (1972) wanaeleza kuwa motisha changamani na uono rafiki kuhusu watu wengine ambao lugha yao ndiyo inafundishwa inaweza kutofautisha fahiwa za mjifunzaji katika vipengele vya kimasikizi vya lugha anayojifunza, na hatimaye kumfanya yeye (mjifunzaji) kuwa mpokezi mzuri wa miundo ya matamshi na kiimbotoni kuliko mjifunzaji ambaye hana uono rafiki kuhusu lugha na wanalugha. Kitu muhimu kinachoongelewa hapa ni mjifunzaji kufanya jitihada kubwa kuelewa lugha na kuitumia pasipo kumtegemea mwalimu.

Tatu, motisha ya ndani na vionjo vya mjifunzaji katika mchakato wa kujifunza inahusu vitu kama vile raghba ya mjifunzaji lugha, kiwango cha utayari wa mjifunzaji Lg2 kushirikishwa katika mchakato wa ujifunzaji huathiri kiwango cha motisha ya ndani. Motisha ya ndani inahusiana na uibuzi na uendelezwaji wa udadisi unaofanywa na mjifunzaji lugha (Ellis, 1997). Chanzo msingi cha motisha ni raghba ya mjifunzaji katika ujifunzaji pamoja na kiwango cha kuridhisha kinachopatikana kutoka katika muktadha wa kujifunzia. Mjifunzaji anayefurahia mchakato wa ujifunzaji lugha huwa imara katika kuelewa stadi za lugha, wakati mjifunzaji ambaye hafurahii mchakato wa ujifunzaji Lg2, uimara wake katika stadi za lugha huwa ni mdogo. Motisha ya mjifunzaji Lg2 inapaswa kuhusishwa zaidi na matokeo na siyo chanzo (Skehan, 1989). Kitu kinachoelezwa hapa na mtaalamu huyo ni kwamba, motisha ndiyo husababisha matokeo mazuri au mabaya ya mjifunzaji lugha na lugha anayojifunza. Mjifunzaji asipokuwa na msukumo thabiti, basi uwezekano wa

kujifunza na kuelewa Lg2 utakuwa na mdogo na akiwa na motisha chanya, atajifunza kwa bidii lugha inayohusika. Hata hivyo, Ellis (2008) na Nahar (2015) wanakubaliana na umuhimu wa motisha katika kuwezesha umilisi wa mjifunzaji, lakini anaongeza kuwa mjifunzaji atafanikiwa ikiwa kanuni bora za ufundishaji zitazingatiwa.

Muktadha wa Kujifunzia

Muktadha wa Kujifunzia ni mazingira halisi ambamo mchakato wa kujifunza lugha hufanyika ukihusisha mfundishaji, mjifunzaji na jamii. Nafasi ya muktadha wa kujifunzia ni muhimu katika kumwezesha mjifunzaji wa Lg2 kupata ingizo. Kulingana na Kreshen (1985) katika Nadhariatete Ingizo ni kuwa ujifunzaji wa Lg2 utatokea ikiwa mjifunzaji wa Lg2 atakuwa amechangamanishwa[1] na lugha ili kupata ingizo ambalo ni la kiwango cha juu kidogo kuliko lile ambalo analo tayari. Krashen anatumia kanuni ifuatayo: i + I, kwa maana ya 'i' inawakilisha kiasi cha lugha ambacho kimekwishaamiliwa na mjifunzaji lugha; na +I inawakilisha kiasi cha lugha (maneno, mifumo ya kisarufi na matamshi) ambayo yako juu kidogo ya yale ambayo mjifunzaji atayapata baada ya darasa linalohusika. Nadhariatete Ingizo inaeleza kuwa ili ujifunzaji wa Lg2 uwe wenye tija, lazima kuwapo na ingizo la kutosha. Mazingira ya kujifunzia mazuri ndiyo yanategemewa kutoa ingizo la kutosha kwa mjifunzaji wa lugha.

Muktadha wa kujifunzia Lg2 hauishii tu katika mazingira ya darasani ambamo ujifunzaji lugha hutendeka, bali unahusisha mazingira ambayo mjifunzaji Lg2 anakaa kama vile nyumbani (Troike, 2012). Hali hii inatokana na kuwa ingizo la lugha la darasani pekee halitoshi kumwezesha mjifunzaji lugha kupata umilisi. Kwa hiyo, muktadha wa kujifunzia lugha unahusu uzingativu wa miktadha mbalimbali ambamo lugha hutumika kwa namna tofauti ijumuishwe darasani. Kwa mfano, lugha ya Kibunge, lugha ya baharia wanaoshusha mizigo na wafanyakazi wa basi, ufafanuzi wake wote ujikite katika muktadha uliopo na unaomzunguka mjifunzaji lugha inayohusika. Muktadha wa kijamii, hasa uzingativu wa utamaduni wa jamii inayohusika kama vile miiko ya jamii inayohusika, lugha ifundishwe kwa kuzingatia mazingira ya jamii, ishara za mikono, mijongeo ya mwili, kusimama kwa mwalimu na kutazama usoni. Mwalimu anatakiwa kuwa na kazi ndogo sana darasani. Wajifunzaji lugha watende zaidi kuliko kusikiliza kwa mwalimu. Ufafanuzi wa vipengele vya kisarufi ufanywe kwa kutumia muktadha wa matumizi kama vile aya au sentensi. Dosari za wajifunzaji lugha zichukuliwe kuwa ni sehemu muhimu ya kujifunza lugha.

[1] Amechanganmanishwa ni tafsiri sisisi ya kisawe cha kiingereza "*Exposed*" kwa maana ya mjifunzaji wa lugha ya pili ya kigeni kuwa katika mazingira ambamo lugha anayojifunza inazugumzwa au kutumika.

Mtazamo

Mtazamo ni jinsi ya kuchukulia mambo au vitu. Ellisi (1985) anaeleza kuwa mtazamo ni imani kuhusiana na vitu fulani katika utamaduni wa lugha anayojifunza, dhidi ya utamaduni wa lugha ya mjifunzaji, madarasa ya kujifunzia, walimu wake na shughuli kuhusu ujifunzaji; ambavyo, kwa kuviamini kwake vinaathiri wajifunzaji na uwezo wao wa kumudu lugha hiyo. Gardner na Lambert (1972) wamechunguza aina mbalimbali za mtazamo na kuainisha katika kategoria kuu tatu, ambazo ni: mtazamo dhidi ya jumuia na watu wanaozungumza lugha ya pili, mtazamo dhidi ya ujifunzaji na kuhusiana na lugha; na mtazamo dhidi ya lugha na ujifunzaji lugha wenyewe kwa ujumla. Kwa hiyo, hali ya kuwa na imani hasi au chanya kuhusu lugha lengwa huathiri hali ya kujifunza lugha inayohusika. Hali ya uhasi huibua ugumu fulani katika kujifunza lugha inayohusika pamoja na utamaduni wake. Mjifunzaji anatarajiwa kuwa na mtazamo chanya dhidi ya lugha na utamaduni wa lugha anayojifunzaji. Mambo haya yakizingatiwa inavyotakiwa, basi ujifunzaji wa Lg2 utakuwa na mafanikio.

Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Modeli ya Elimu Kijamii ya Gardner (1985) ambayo ni sehemu pana ya Nadharia ya Motisha ya Ujifunzaji. Modeli hii inachukulia kuwa ujifunzaji wa Lg2 ni mchakato unaohusisha mambo mengi yaliyo ndani na nje ya mjifunzaji. Kiini cha mafanikio katika kujifunza Lg2 ni motisha aliyonayo mjifunzaji wa lugha inayohusika. Msukumo binafsi alionao mjifunzaji wa kujifunza lugha inayohusika ndiyo kiini cha kupata umilisi wa kimawasiliano wa lugha anayojifunza. Hoja hii ina maana kuwa mjifunzaji mwenye msukumo wa ndani ndiyo mwenye uwezekano wa kujifunza na kumudu lugha vizuri tofauti na yule mwenye motisha ya nje. Gardner (1985) anabainisha kuwa motisha katika ujifunzaji wa Lg2 ni mchanganyiko wa jitihada, nia ya kutaka kufanikiwa kulingana na malengo pamoja na mtazamo chanya dhidi ya lugha unayojifunza. Modeli ya Elimu Kijamii inatambua nafasi ya motisha katika kujifunza jambo lolote ikiwa ni pamoja na lugha. Wazo hili lilichukuliwa kwa uzito mkubwa katika utafiti huu. Wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda wanamtazamo upi katika kujifunza Kiswahili. Mtazamo walionao wajifunzaji wa Kiswahili nchini Uganda unaweza kuwa na athari katika idadi ya wajifunzaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere.

Uwasilishaji wa Data

Lengo la jumla la utafiti huu lilikuwa kuchunguza sababu za kuwapo idadi ndogo ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere nchini Uganda. Katika kutimiza lengo hilo, utafiti ulifanya mahojiano ya wazi na walimu wanaofundisha Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Makerere na wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika chuo hicho hicho cha Makerere. Maoni ya jumla yaliyopatikana kwa watoa taarifa wa pande zote mbili ni kuwa lugha ya Kiswahili

inatazamwa kama lugha ya watu wezi na inayotumiwa na wanajeshi kutesa na kunyanyasa watu. Hivyo, watu hawako tayari kujifunza lugha ya kutesea na kuwaibia watu. Watoa taarifa walipohojiwa walithibitisha kwa mifano mbalimbali inayotumiwa na wezi wakiingia katika makazi ya watu wakitumia lugha ya Kiswahili. Baadhi ya tungo za Kiswahili zinazotumiwa na wezi zimeoneshwa katika sehemu hii. Mfano 1 unahusu tungo za wezi:

i. Fungua mlango
ii. Lala chini
iii. Lete pesa

Chanzo: Uwandani (2018).

Kwa mujibu wa watoa taarifa, wezi hutumia kauli hizi kudai nan kupora mali. Walipoulizwa zaidi kwa nini wanadhani wezi hupendelea kutumia Kiswahili, majibu ilikuwa ni kwamba, lugha ya Kiswahili hutumika kuficha lafudhi ya wahusika. Kwa hiyo, jamii inachukulia hasi lugha ya Kiswahili kwa sababu hiyo. Aidha, watoa taarifa walibainisha misemo mbalimbali ambayo huitumiwa nawanajeshi au polisi wanapokuwa kazini na kutaka kuonesha nguvu za mamla walizo nazo na kutesa raia. Mfano 2 unahusu Tungo za Askari:

i. Chapa viboko
ii. Kanyaga mguu
iii. Ondoka hapa
iv. Maliza yeye

Chanzo: Uwandani (2018).

Pia, walifafanua kuwa wanajeshi hutumia lugha ya Kiswahili kwa sababu watu wengi nchini Uganda hawaifahamu lugha ya Kiswahili, Hivyo, hutumia ili kuwaficha raia wasiijue na wasielewe kwamba wanatakiwa kufanya nini na kujikuta wanateswa. Watoa taarifa wengine walielezwa kwamba Waganda hawachagui kusoma somo la Kiswahili katika Vyuo Vikuu kwa sababu ni lugha ambayo hutumiwa na madereva taksi kukatalia chenji iliyobaki. Sehemu ya mazungumzo na mtoa taarifa alisema kuwa Kiswahili kinahusishwa na unyanyasaji wa wezi na askari. Pia, hutumiwa na madereva tax ambao ukiwapa hela kubwa na ukitakiwa kurudishiwa chenji hutumia Kiswahili ili kudhulumu na kuwalaghai wananchi. Alifafanua zaidi kwamba wakati anasema maneno hayo ya Kiswahili, tayari anawasha gari na kufunga kioo; kisha kuondoka. Mfano 3 ni tungo za Kiswahili zinazotumiwa na Madereva Taksi:

i. Imeisha (Hela uliyotoa imeisha)
ii. Hakuna baki (Hakuna salio kwangu)
iii. Nenda wewe (Toka ndani ya gari)

Chanzo: Uwandani (2018).

Tungo 3 hapo juu zinavyoashiria namna dereva taksi akimwamuru abiria wake kutekeleza yale anayomwambia. Tungo hizo zinaonesha kuamuru tu. Maneno yaliyo katika mabano ni ya mtafiti kwa ajili ya ufafanuzi. Hivyo, Kiswahili kinasababisha udhulumaji ndiyo maana watu wengi hawataki kusoma na hata wazazi hawaruhusu watoto wao kusoma Kiswahili katika ngazi za sekondari.

Jedwali Na. 1.2: Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Na.	**Semi Mbaya zinazotumika wanajamii**	**Kundi la watu linatumia semi hizo**
1.	Imeisha	Madereva taksi
2.	Hakuna baki	Madereva taksi
3.	Nenda wewe	Madereva taksi
4.	Maliza yeye	Wanajeshi/Jeshi la Polisi
5.	Ondoka hapa	Wanajeshi/Jeshi la Polisi
6.	Kanyaga mguu	Wanajeshi/Jeshi la Polisi
7.	Chapa viboko	Wanajeshi/Jeshi la Polisi
8.	Fungua mlango	Wezi/Majambazi
9.	Lala chini	Wezi/Majambazi
10	Lete pesa	Wezi/Majambazi

Chanzo: Uwandani (2018).

Mifano katika jedwali Na. 1.2 kama inavyoonesha hapo juu, Kiswahili hutumiwa na makundi makuu matatu ya madereva taksi, Jeshi la Polisi na majambazi. Watoa taarifa wanadai hawakutegemea kundi la polisi au wanajeshi kutumia tungo mbaya za Kiswahili kulingana na majukumu yao. Hivyo, matumizi ya tungo za kutweza utu zinazofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama wa taifa kwa kutumia lugha ya Kiswahili kumesababisha jamii pana ya Wanauganda kukichukia Kiswahili na kutotaka kabisa kujifunza. Ubaya unaojitokeza kwa kundi hili ukihusishwa na lugha ya Kiswahili ni kuwa askari hubadili lugha kutoka ama Kiingereza au Kiganda alichokuwa anazungumza mwanzo pale anapotaka kumshughulikia au kumdhuru raia. Hivyo, Kiswahili kinachukuliwa kuwa ni lugha ya watu wabaya na makatili. Kauli kama "*Maliza yeye*" kwa maana ya ua kabisa na kauli kama "*Chapa viboko*" au "*Kanyaga mguu*" zinazodaiwa kutolewa na askari dhidi ya raia ndiyo zinafanya wananchi wengi wa Uganda kuhusisha moja kwa moja lugha ya Kiswahili na ukatili. Uhusishaji huu unatokana na askari kubadili msimbo kutoka lugha ya ama Kiingereza au Kiswahili aliyokuwa akizungumza awali na kutumia Kiswahili kuashiria kuwatesa kwa raia. Waganda hawana motisha ya kujifunza lugha ya Kiswahili katika ngazi ya Vyuo Vikuu. Hali hii inasababishwa na athari za kijamii wanazopata kutoka kwa wale wanaojua na kukitumia Kiswahili nchini humo.

Kwa upande mwingine, wezi na majambazi wanaovamia nyumba za watu, hasa nyakati za usiku kutumia kauli za kuamuru kwa Kiswahili kwa yeyote aliyemo ndani kama vile "*Fungua mlango*", "*Lala chini*" na "*Leta pesa*". Watoa taarifa walieleza kuwa hizo ndizo sababu zinazowafanya wananchi wengi wa Uganda kukichukia Kiswahili. Walipohojiwa wanafikiri ni kwa nini wezi na majambazi hutumia lugha ya Kiswahili, watoa taarifa, hasa wanafunzi wa shahada za Umahiri, walisema wezi hutumia lugha ya Kiswahili ili kujificha wasitambulike. Kutumia lugha ya Kiganda au Kiingereza inaweza kuwa rahisi kuwatambua kwa kusikiliza sauti zao. Kutumia Kiswahili, ambacho Waganda wengi hawakijui inakuwa ni vigumu kubaini sauti hizo. Hivyo, kwa kuwa kundi hili ovu hutumia Kiswahili katika kutekeleza uovu wao, jamii pana ya Waganda wamekichukia Kiswahili na kwamba hawako tayari kuwaruhusu watoto wao kujifunza lugha ya Kiswahili.

Kuhusu madereva taksi, kwa mujibu wa watoa taarifa, madereva taksi na makondakta wakitaka kutorudisha chenji hutumia lugha ya Kiswahili. Ifahamike kwamba, dhana ya taksi katika muktadha wa Uganda inahusu gari za abiria za umma zinazofirisha watu katika miji muhimu ya kibiashara kama vile Kampala na Entebe. Kulingana na watoa taarifa, madereva taksi na makondakta pale wanapotaka kutorudisha baki ya nauli hutumia kauli za kuamuru kwa abiria wao kwa kuwambia; "*Imeisha*", "*Nenda wewe*" na "*Hakuna baki*". Watoa taarifa walifafanua kuwa kauli hizi hazitumika kwa kutumia lugha ya ama Kiingereza au Kinganda ambazo ni lugha kuu za mawasiliano nchini humo. Hivyo, hali hii huwafanya wanajamii wa Uganda kuona kuwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya kidhulumaji. Jambo hili huchochea kutokuwa na wanafunzi wengi wanaosoma Kiswahili katika shule za sekondari kuna uhusiano wa moja kwa moja na idadi ndogo ndogo ya wanafunzi wanaojiunga kusoma Kiswahili katika vyuo vikuu.

Mjadala na maoni

Jamii pana inapokuwa na mtazamo hasi dhidi ya lugha ambayo wajifunzaji hujifunza, mbali na kupungua idadi ya wajifunzaji madarasani; hata hao wao wachache uwezekano wa kumudu lugha hiyo huwa ni mdogo sana. Hali ya kushindwa inatarajiwa kutokea kutokana na wanajamii wengi walio nje ya madarasa kutoshirikiana na wajifunzaji lugha inayohusika. Mjifunzaji lugha kukosa kupata ushirikiano kwa jamii pana inayomzunguka humpunguzia mjifunzaji lugha huyo kupata ingizo la lugha. Kukosekana kwa ingizo katika mazingira ya kujifunzia na ujifunzaji hushusha motisha ya kujifunza lugha. Mjifunzaji lugha motisha inaposhuka uwezekano wa kujifunza na kumudu lugha hiyo huwa ni mdogo sana. Hivyo, ikiwa jamii ya Waganda hawawavutii watoto kujifunza lugha ya Kiswahili, hata hilo kundi dogo linalijifunza kwa sababu zao mbalimbali hawawezi kumudu lugha hiyo kwa kiwango karibu sawa na wazawa. Juhudi kubwa zinatakiwa kufanywa na wadau wa lugha ya Kiswahili wa ndani na nje ya Uganda yanatakiwa

kufanya warsha za kitaifa nchini ili kuondoa dhana hii potofu iliyojengeka miongoni mwa wananchi wa taifa hilo. Kwa hali ilivyo sasa, mpango wa serikali ya Uganda kuhusu Kiswahili kuwa lugha ya pili nchini humo ifikapo 2020 hautafanikiwa.

Hitimisho

The findings reveal that Social Studies teachers failed to prepare and using T/L materials due to, work loaded, financial constraints and the pupils suffered the most by missing the investigative activities of the historical sites and museums around their environments which would address the shortage were not enough.

Social Studies Teachers' Knowledge of Assessing Pupils Learning in the Classroom

This part wanted to know how and when Social Studies teachers assessed/L processes. The findings show that procedures employed by Social Studies teachers to assess pupils while the lesson was in progress. However, the process did not help pupils towards enhancing abilities, skills, creativity and critical thinking when responding to questions. The pupils were asked, question but failed to answer the question and remained quiet. Then, through lecture, a teacher continued teaching. Toward the end of the lesson, the teacher wrote five questions on the chalkboard as homework. The findings revealed that Social Studies teachers were normally assessing pupils through questions and answers during and at the end of the T/L processes. This raised a concern that teachers did not allow pupils to comment on concepts, disagree or raise more questions about the lesson. Hence, the interactions between pupils and the lesson did not provide opportunities for teachers to evaluate the extent to which the lesson was whether clear to pupils or not. The findings from the interviews with teacher TB claimed that, I assess pupils during the process of teaching whereby I provide exercise on the contents covered.

The findings indicate that in Tanzania Social Studies teachers seemed to have limited instructional competences, pedagogies, experiences, knowledge, information and skills in teaching of Social Studies. Also, they lacked practical evidence to connect between classroom interactions and pupils' life experiences, knowledge, observations and skills. This is contrary to the Social Studies Basic Education Curriculum (BEC)'s of 2016 expectations for standard III-VI and the current (CBC) that recommend LCA (MoEST, 2016). Social Studies teachers demonstrated that the T/L Social Studies has a limited T/L material against the demands of Social Constructivist Theory which demands environments rich in teaching resources. The findings agree with the studies by Kopweh (2014) which reported a similar situation that T/L materials in Tanzanian schools are insufficient. This is in contrast with the study by Okobia (2011) which stated that T/L materials are essential to ensure that the new curriculum and syllabus are well implemented. Similarly, in depth-learning occurs when pupils construct knowledge through T/L materials rather than quickly moving from topics to topics. Social Studies teacher background appeared to hinder the assessment and evaluation of the T/L processes. The findings revealed that Social Studies teachers did not have instructional competences to assessing and diagnosing pupils learning progress as recommended in the Social Studies curriculum. The curriculum requires teachers to act as facilitators, coach and mentors of pupils learning through supervision and of the degree to which set of objectives are achieved by looking at activities done by pupils.

Conclusions and Recommendations

Based on the study findings, Social Studies teachers did not fully demonstrate the instructional competences required for enhancement of pupils as recommended by Social Studies curriculum and the literature. This signified that Social Studies teachers were not competent enough to identify the important tasks to accomplish, examine alternative ways to accomplish the objectives, establish adequate resources to assist in achieving goals and process of assessing the outcome of the plan to help pupils acquire the expected Social Studies competences. As a result, pupils had limited opportunity to participate in instructional activities during the teaching and learning processes. Besides, Social Studies teachers failed to plan and prepare different learning activities through which pupils could construct new knowledge to acquire the expected subject competences. Social Studies teachers face various challenges (shortage of teaching and learning materials, lack of preparation) which hindered their ability to demonstrate instructional competences which embrace learner-centred teaching methods.

It is thus recommended that professional development initiatives should be undertaken to support Social Studies teachers with instructional competences. There is a need for MoEST to ensure teachers are equipped with relevant pedagogical and content knowledge demonstrated in the curriculum to build teachers' pedagogical competences, creativity and interest. Since the study was delimited on investigating Teachers instructional competences for teaching Social Studies to primary schools pupils in Tanzania while limiting to six primary schools in Rungwe district, it is recommended that a more comprehensive study be conducted to include more schools, districts and the use of both public and private schools to have reliable information on Social Studies teachers' instructional competences.

References

Ada, J. H., & Azisah, S. (2016). The Contribution of Teachers' Pedagogical Competence toward the Effectiveness of Teaching of English at Mtsn Balang-Balang. *Eternal (English, Teaching, Learning and Research Journal), 2* (2), 238-251.

Adeyemi, B. A. (2016). The Efficacy ff Social Studies Teachers' Competence in the Use of Play Way Method in Lower Primary Schools in Osun State, Nigeria. *Journal of Education and Human Development, 5* (1), 249-255.

An, S. (2017). Preparing Elementary School Teachers for Social Studies Instruction in the Ontext ff Edtpa. *The Journal of Social Studies Research*, *41* (1), 25-35.

Akhtar, S. (2008). The Implementation of Education for Citizenship in Scotland: Recommendation of Approaches for Effective Practice. *Improving Schools, 11* (1), 33-48.

Bakhuru, K.M. (2015). Competencies for Effective Managementteaching- Perception of Teachers and Administrators of Indian B-School. *Journal of Economic and Management, 2* (7) 1-7

Ben-Peretz, M. (2011). Teacher Knowledge: What Is It? How Do We Uncover It? What Are Its Implications for Schooling? *Teaching and Teacher Education, 27* (1), 3-9.

Ciullo, S., Falcomata, T., & Vaughn, S. (2015). Teaching Social Studies to Upper Elementary Students with Learning Disabilities: Graphic Organizers and Explicit Instruction. *Learning Disability Quarterly, 38* (1), 15-26.

Crick, R. D. (2008). Key Competencies for Education in a European Context: Narratives of Accountability or Care. *European Educational Research Journal, 7*(3), 311-318.

Crifford, O. E. (2013). Social Sstudies Teachers' Competency Need for Effective Implementation of Universal Basic Education Program. Nigeria. *Journal ff Social Studies and Civics Education, 3* (1), 21-38.

Curry, K., & Cherner, T. (2016). Social Studies in the Modern Era: A Case Study of Effective Teachers' Use of Literacy and Technology. *The Social Studies, 107* (4), 123-136.

Creswell, J. W. (2012). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approach*. Los Angeles: SAGE Publications.

Creswell, J. W. (2014). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approach*. California: SAGE Publications.

Cooper, D. G. (2015). The Lesson Observation On-line (Evidence Portfolio) Platform. *Australian Journal of Teacher Education, 40* (1), 83-93.

Denscombe, M. (2014). *The Good Research Guide: For Small-Scale Social Research Pprojects*. UK: Mcgraw-Hill.

District School Quality Assurer. (2019). Primary Schools Quality Assurer Report. Rungwe, Tanzania.

Komba, S. C., & Mwandanji, M. (2015). Reflections on the Implementation of Competence Based Cuurriculum in Tanzanian Secondary Schools. *Journal of Education and Learning, 4* (2) 73-80.

Kopweh, S. K. (2014).*Curriculum Development in Tanzanian Investigation of the Formulation, Mmanagement and Implementation of the 2005 Curriculum Reform in Selected Disadvantaged Districts*. Unpublished Doctoral Dissertation, Glasgow University, Scotland.

Kunter, M., Klusmann, U., Baumert, J., Richter, D., Voss, T., & Hachfeld, A. (2013). Professional Competence of Teachers: Effects on Instructional Quality and Student Development. *Journal of Educational Psychology*, *105* (3), 805-820.

Ministry of Education Science and Technology [Moest] (2016). *Social Studies Syllabus for Basic Education Standard 111-VI*. Dar Es Salaam, Tanzania: TIE.

Ministry of Education and Culture (1995). *Education and Training Policy.* Dar Es Salaam, Tanzania: Author.

Meena, W. E. (2009). *Curriculum Innovation in Teacher Education: Exploring Conceptions among Teacher Educators*. Unpublished Doctoral Thesis, Åbo: Åbo-Akademi University, Finland.

Mtitu, E. A. (2014). *Learner-Centred Teaching in Tanzania: Geography Teachers' Perceptions and Experiences*. Unpublished Doctoral Thesis, Victoria University if Wellington Australia.

Nywage, E. G. (2007). *Specialization in Teaching Subject at Primary School Level In Tanzania: An Investigation on The Effective of Training And Posting In Rungwe District.* Unpublished Masters of Education Dissertation, University of Dar Es Salaam, Tanzania.

Okobia, E. O. (2011). Availability and Teachers' Use of Instructional Materials and Resources in the Implementation of Social Studies in Junior Secondary Schools in Edo State, Nigeria. *Review of European Studies*, *3* (2), 90-98.

Oliver, P. F. (2001). *Developing the Curriculum*. United State of America: Priscilla McGeehan.

Parker, W. C. (2015). *Social Studies to day*. (2rd Ed). New York, NY: Rutledge.

Priestley, M. (2011). Schools, Teachers and Curriculum Change: A Balancing Act? *Journal of Educational Change*, *12* (1), 1-23.

Ritter, J. K. (2012). Modelling Powerful Social Studies: Bridging Theory and Practice with Preserves Elementary Teachers. *The Social Studies*, *103* (3), 117-124.

Shah, S. R., & Al-Bargi, A. (2013). Research Paradigms: Researcher's Worldviews, Theoretical Frameworks and Study Design. *Arab World English Journal*, 4 (4) 252-264.

Sumra, S. (2007). *What Has Been Achieved in Primary Education? Key FIndings from Overnment Reviews*.Dar es Salaam: HakiElimu.

Sekaran, U., & Bougie, R. (2016). *Research Methods for Business: A Skill Building Approach*. Canada: John Wiley & Sons.

Ukpokodu, O. N. (2020). Marginalization of Social Studies Teacher Preparation for Global Competence and Global Perspectives Pedagogy: A Call for Change. *Journal of International Social Studies*, *10* (1), 3-34.

United Nations Scientific and Cultural Organization (UNESCO). (2010). *World Data on Education.* United Republic of Tanzania: Author.

Dhamira katika Nyimbo za Ali Salehe Kiba: Mifano Kutoka katika Wimbo wa '*Msiniseme*'

Omary Mohamed Maguo
Idara ya Isimu na Fasihi,
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Omarymohamed36@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imeangazia dhamira zilizomo katika wimbo wa '*Msiniseme*' wa Ali Kiba. Makala imekuja ili kujibu hoja iliyotolewa na wasanii mbalimbali kuwa wimbo huo hauelezi mambo ya msingi, lakini ulipewa nafasi kubwa katika vyombo vya habari. Hoja hii ilitolewa mnamo mwaka 2010 katika Kongamano la Bongo Fleva lilifanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Miaka nane baadaye, tumeona kuwa ipo haja ya kuishughulikia kwa kuichunguza hoja hiyo kwa kuonesha na kueleza mambo ya msingi yaliyomo katika wimbo teule, licha ya kuwa unanukuliwa na kutazamwa kama hauakisi mambo yanayoihusu jamii moja kwa moja. Uchunguzi wa makala hii umeichukulia fasihi kuwa ni kitengo pekee kilicho na uwezo wa kuakisi sayansi na utamaduni wa jamii unaodhibitiwa na miundo iliyopo katika kijamii inayohusika. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa mkabala wa kimaelezo. Uchambuzi na uhakiki wa data zilizowasilishwa katika makala hii umeongozwa na nadharia ya Simiotiki. Makala hii imebaini kuwa kuwapo kwa dhamira mbalimbali zenye tija kwa maana ya kuielimisha jamii katika nyanja zake zote za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Utangulizi

Muziki wa Kizazi Kipya maarufu kwa jina la Bongo Fleva umekuwa na kuimarika zaidi katika miaka ya hivi karibuni kutokana na kutoa kwake ajira kwa vijana wengi wa Kitanzania na Afrika ya Mashariki kwa jumla. Kukua kwa muziki huu kumechangiwa na kuibuka kwa wasanii wengi chipukizi na wakongwe ambao kila uchao hutunga na kuimba nyimbo zenye maudhui kulingana na malengo yao mahsusi. Katika hali ya kawaida ni vigumu sana kutomtaja msanii Ali Salehe Kiba (King Kiba) unapozungumza juu ya wasanii waliochangia katika kuukuza muziki wa Bongo Fleva. Wapo wasanii wanamtazama Kiba kama mtu mwenye kipaji cha pekee kutokana na umahiri wake katika fani ya muziki. Kutokana utunzi na uimbaji wake uliotukuka amefanikwa kupata tuzo mbalimbali, hasa ya kuwa 'Msanii Bora wa Afrika ya Mashariki ya Mwaka 2011'. Mwaka 2015 alishinda tuzo tano za '*Kili Awards'* na tuzo ya MTV ya kimataifa. Mwaka 2016 alipata mkataba wa kufanya kazi na kampuni ya kimataifa inayojishughulisha na muziki inayoitwa '*Sony Muzic*

Entertainment'. Baadhi ya nyimbo zake ni 'Aje', '*Chekecha Cheketua'*, '*Nagharamia*', '*Nisamehe*', '*Cinderella*', '*Msiniseme*' na '*Kipusa*'. Makala hii imeuteua wimbo wa '*Msiniseme*' ili kukidhi lengo mahsusi la uchunguzi.

Dhana ya Bongo Fleva

Bongo Fleva linatokana na maneno mawili 'Bongo' kwa Kiswahili na 'Flavor' kwa Kiingereza (Askew, 2002). Bongo ikiwa na maana kuwa ili mtu aweze kumudu maisha katika jiji la Dar es Salaam lazima awe akili na maarifa mengi, vinginevyo ataishia kulala na njaa. Hali hii ikalifanya pia jiji la Dar es Salaam na sasa Tanzania kufahamika kwa jina la Bongo. Ukisikia mtu kutoka mkoani anasema anakwenda Bongo, mtu huyo anakwenda Dar es Salaam na aliyepo nje ya nchi anaposema anakwenda Bongo ana maana kuwa anakwenda nchini Tanzania. Neno Fleva lina maana ya 'Ladha' kama ilivyo katika lugha ya Kiingereza. Aidha, 'Bongo Fleva' maana yake ni 'Ladha za Bongo' yaani, 'Muziki wa Tanzania wa Vijana. Muziki wa Bongo Fleva hujumuisha aina na mitindo anuai kama vile ya Reggae ya Tanzania, Ragga, Bongo Bangla, TAKEU, Hip Hop na Rymes na Blues na (Perullo na Fenn, 2003).

Bongo Fleva ni mchanganyiko wa vionjo kutoka muziki wa Marekani wa Hip Hop, R & B, Zouk, Reggae, Congo Lese Bolingo, muziki wa India na Tanzania (Suriano, 2006). Muziki wa Bongo Fleva umechota vionjo kutoka aina mbalimbali za muziki duniani; na kadri muda unavyokwenda ndivyo unavyoendelea kujibainisha zaidi kuwa ni muziki wa Kiafrika (Suriano, 2007). Miaka ya 1990 nyimbo hizo zilianza kufahamika kwa watu wengi zilionekana kuwa ni za Kimarekani kutokana na uimbaji, uvaaji, uteuzi wa maneno na uchezaji jukwaani. Nyimbo hizo zilitazamwa kama ni za kihuni kwa sababu zilisheheni utamaduni wa kigeni kuliko wa Kitanzania (Omari, 2009). Katika kipindi hiki nyimbo hizo zinatazamwa kama sehemu muhimu ya ajira kwa vijana. Dhana ya kwamba ni muziki wa wahuni sasa imeendelea kupungua na kutoweka kabisa (Omari, 2011).

Lengo la Makala

Makala hii imelenga kuchunguza dhamira zilizomo katika wimbo wa '*Msiniseme*' wa Ali Kiba ulitoka kwa mara ya kwanza mwaka 2009. Wimbo huu ulizua gumzo kubwa katika Kongamano la Muziki wa Bongo Fleva lililofanyika mwaka 2010 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Gumzo hilo liliibuliwa na wasanii ambao hawakuona sababu za msingi za wimbo huo kupewa nafasi kubwa katika vyombo vya habari kwa kuwa hawakuona umuhimu wa maudhui yake ya kwa jamii. Takribani, miaka kumi sasa lilipotokea gumzo kuhusu nafasi ya wimbo huo tangu kufanyika kwa kongamano hilo. Katika taaluma ya fasihi, hakuna mtaalamu yeyote aliyeshughulikia wimbo huo ili kupata majibu ya gumzo lililowahi kuibuka kuhusu

dhima ya wimbo uliobainishwa. Makala hii imeshughulikia pengo hilo kwa kuchambua dhamira zilizomo katika wimbo teule.

Methodolojia

Utafiti huu umeongozwa na mbinu ya uchunguzi kifani Data za utafiti zimekusanywa kutoka katika wimbo '*Msiniseme*' kwa mbinu ya usomaji makini. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kupakua wimbo teule mtandaoni. Hatua ya pili ikawa ni kusoma wimbo unaohusika na kudondoa maneno, msitari au ubeti ambao tuliona kuwa umebeba dhamira muafaka kulingana na lengo mahsusi la makala hii. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuunda dhamira ili uchambuzi ufanywe kwa namna ambayo italeta mantiki. Baada ya zoezi la kukusanya data kukamilika ndipo tukazichambua kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Mkabala wa kimaelezo hutumika kuchambua data kwa kuzitolea mantiki ambayo yanaumana na lengo mahsusi la kazi inayohusika (Berg, 2009). Data zimedondolewa kutoka katika wimbo teule zilichambuliwa kwa maelezo yaliyoimarishwa na nadharia ya Simiotiki.

Mkabala wa Kinadharia

Makala hii imetumia nadharia ya Simiotiki katika uchambuzi wa dhamira zinazojengwa katika wimbo wake wa '*Msiniseme*'. Simiotiki ni nadharia inayoangazia matumizi ya misimbo, ishara, picha, taswira na mafumbo katika kazi ya fasihi (Umberto, 1976 & Barthes, 1994). Ili kuweza kuelewa dhamira ndani ya kazi yoyote ile ya kifasihi ni lazima mchambuzi afahamu matumizi ya lugha iliyotumika. Imekuwa ni jambo jepesi kwa baadhi ya wasanii kudahili kuwa wimbo wa '*Msiniseme*' hauna maana yoyote kwa sababu hawakutumia nadharia ya Simiotiki katika kuuchambua wimbo huu. Nadharia hii iimeundwa kutokana na misimbo ya kimatukio, kiseme, kiutamaduni, kiishara na kihemenitiki (Mark, 1995). Misimbo hujibainisha kwa namna mbalimbali, hasa msanii wa kazi ya fasihi anapotumia mbinu za kisanaa kuwasilisha dhamira alizozikusudia.

Katika makala hii, mtafiti aliitumia nadharia ya Semiotiki katika uchunguzi wa dhamira katika wimbo wa '*Msiniseme*' wa Ali Kiba. Kwa mujibu wa Chandler (1992), hadhira hutengeneza maana ya kazi fulani ya fasihi kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya ishara zilizotengenezwa na msanii. Aidha, utengenezaji wa maana hutegemea sana muktadha wa mnyambulishaji wa taswira zinazotumika katika kazi inayohusika. Mtafiti aliitumia nadharia hii kuzichunguza ishara, picha na taswira zilizomo katika wimbo wa 'Msiniseme' ili kubaini dhamira zilizomo kulingana na lengo mahsusi la utafiti. Kipekee, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kwa niaba ya kitu kingine (Solomon, 1988). Huu ndio msingi wa uteuzi wa nadharia ya Semiotiki iliyochunguza kipengele cha dhamira katika wimbo uliolengwa katika makala hii.

Dhamira katika Wimbo Teule

Dhamira huelezwa kama mawazo makuu ya mtunzi wa kazi ya fasihi ambayo anataka hadhira yake iyafahamu (Njogu na Chimerah, 1999). Katika kazi ya fasihi huwa na dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Kwa kawaida, dhamira kuu hujengwa na zile ndogo ndogo. Wimbo wa '*Msiniseme*' ni kazi ya fasihi inayojibainisha kupitia utanzu wa ushairi katika kipera cha nyimbo. Hivyo, wimbo huu una dhamira ndani yake tulizozidhamiria kuzibainisha. Kama tulivyokwishaeleza mahali fulani katika makala hii, wimbo huu ulitajwa na kujadiliwa kuwa hauna mashiko yoyote, lakini umepewa nafasi kubwa katika vyombo vya habari. Kupitia sehemu hii tumekusudia kuonesha kuwa wimbo huu una mashiko na kupewa nafasi kubwa katika vyombo vya habari kwa wakati huo ilikuwa ni sahihi. Kabla ya kuanza uchambuzi ni vema tuuwasilishe wimbo teule wa '*Msiniseme*':

Kiitikio:

1. Msinisemee ah, msinisemee ah,
2. Msinisemee ah, msinisemee ah,
3. Kama napenda nakula,
4. Msinishangae, msinishangae,
5. Msinishangae, msinishangae,
6. Kama napendwa kula.

Ubeti wa Kwanza:

7. Basi hivi juzi juzi,
8. Kulikuwa na shughuli,
9. Mtaa wa pili tena si mbali,
10. Kulikuwa na pilau na wali,
11. Basi nami nikajiunga,
12. Pale pale kupiga mpunga,
13. Watu wakajipanga,
14. Nikaanza kwa tonge na nyama,
15. Ni nyama tonge, ni nyama tonge,
16. Ni nyama tonge mpaka wakanifukuza,
17. Nikasema sijali, nikatoa pesa mfukoni,
18. Nikanunua mayai, kilichofuata watu hawakai.

Ubeti wa Pili:

19. Ilikuwa Jumapili,
20. Siku ya watu wenye ufahari,
21. Kujirusha sehemu mbalimbali,
22. Nami nikasema leo sikubali,
23. Wacha niendee, wacha niendee,
24. Wacha niendee, ila pesa sina nataka nikale,
25. Nikapita sokoni,

26. Nikaomba embe sokoni,
27. Nikaelekea baharini,
28. Nikawaona wengi ufukweni,
29. Napita na embe kiutani,
30. Nakula ili watamani,
31. Mate yaliwajaa midomoni,
32. Basi wote wakaanza kuniomba,
33. Msiniombee, msiniombee,
34. Msiniombee, si mnasema,
35. Mimi napenda kula.

Huu ndio wimbo wa '*Msiniseme*' ambao umeundwa kwa beti mbili kama tulivyoziainisha hapo juu. Wimbo huu umesheheni dhamira mbalimbali, lakini ukitazama kwa haraka haraka utaishia kusema kama vile walivyosema wasanii kuwa hauna maana yoyote ya msingi zaidi ya mtunzi mwenyewe kujisifu kuwa anapenda kula. Baadhi ya dhamira zilizojadiliwa katika makala hii zimebainishwa katika sehemu hii.

Rushwa na Ufisadi

Rushwa ni kitendo cha mtu au kundi la watu kutoa kitu fulani kwa lengo la kupata haki au upendeleo fulani (Mpangala, 2007). Inawezakana kabisa ni haki ya mtu kupatiwa huduma fulani kama vile hospitalini, mamlaka ya mapato, mahakamani, huduma za maji, umeme, pembejeo na huduma nyinginezo, lakini hapewi huduma hizo mpaka atoe rushwa. Pia, rushwa hujitokeza katika miradi mikubwa ya serikali kama vile utoaji wa tenda za ujenzi na manunuzi, utoaji wa vibali vya uchimbaji na usafirishaji wa madini na miradi mingine mikubwa. Kupitia kiitikio cha wimbo huu, mtunzi anaonesha kuwa rushwa ilianza kuonekana kuwa ni kitu cha kawaida. Katika msitari wa 3 na 6 kunarudiwa maneno, '*Kama napenda kula'*, ikiwa na maana kuwa rushwa ilikuwa ni jambo la kawaida. Matumizi ya neno "kula" yametumika kimsimbo wa kimatukio kurejelea tukio la kutoa na kupokea rushwa.

Katika miaka hiyo ambao wimbo huu ulitungwa ilikuwa ni kawaida kwa mtu kuchukua rushwa na kujijengea maisha mazuri. Ilifika mahali kiongozi wa umma ambaye alimaliza muda wake wa uongozi akiwa na hali mbaya kimaisha watu walimcheka kuwa alikuwa mjinga kwa kuwa hakuwa akijihusisha na vitendo vya rushwa ili kujinufaisha zaidi. Mtunzi wa wimbo '*Msiniseme*' anaiwasilisha hali hiyo akiwa na maana kuwa wale watu wachache ambao wanaonekana kuwa ni wapinga rushwa wasifanye hivyo kwani kupokea rushwa kutamfanya mtumishi kuwa na maisha mazuri ili baadaye asichekwe na wanajamii. Msitari wa 1, 2, 4, 5, 7 na 8 inaonesha kuwa kuna uhalali fulani wa kupokea rushwa. Hii inatokana na mistari hiyo kusisitiza kuwa mchukua rushwa asisemwe wala asitengwe kwa sababu anapenda rushwa.

Katika ubeti wa kwanza msanii anaonesha kuwa rushwa ni kitu ambacho kinapendwa na watu wengi, ingawa wapingaji wake ni wachache. Msitari wa 13 mpaka 22 unashadadia hoja kuwa rushwa ni kitu ambacho kilikuwa kimeota mizizi katika jamii. Matumizi ya maneno "Pilau na wali" katika msitari wa 13 yamejengwa kutokana na msimbo wa kiishara kuonesha kuwa rushwa ni kitu ambacho kilipendwa sana na watu. Pilau na wali ni aina ya chakula kinachopendwa sana na wanajamii. Baadhi ya wanajamii hupata aina hii ya chakula siku za sikukuu tu au misiba kwa watu wenye fedha. Hapa, pilau na wali vimetumika kurejelea namna rushwa ilivyopendwa na kukumbatiwa kama aina hii ya chakula. Katika msitari wa 17 msanii anaonesha kuwa wapenda rushwa walifikia mahali wakawa hawana huruma tena kwa wananchi kwani walipokea rushwa kubwa kiasi cha kudumaza maendeleo ya jamii. Msitari huo unasema, "*Nikaanza kwa tonge na nyama*" ikiwa na maana kuwa pale kunapokuwa na miradi ya maendeleo baadhi ya wasimamizi wa miradi hiyo hufikiria namna watakavyojinufaisha wao binafsi kabla hata ya kutafakari ni kwa vipi mradi fulani utajengwa au kukamilishwa kwa kiwango kinachopaswa ili uwakomboe wananchi katika umasikini. Kitendo cha kuchukua kila tonge na nyama yake ni ishara ya dhuluma dhidi ya mali ya wananchi kwa maslahi yao binafsi.

Baada ya kuonekana rushwa imeshika mizizi mpaka upatikanaji wa maendeleo kwa wananchi umekuwa ni kitendawili, ndipo taasisi zinazohusika zilipoanza kupambana ili kutokomeza rushwa. Hili linajibainisha katika msitari wa 19 anaposema, "*Ni nyama tonge mpaka wakanifukuza*". Kauli hii imejengwa kwa msimbo wa kiishara ikiwa na maana kwamba wapambanaji na wadhibiti wa rushwa wamechukua nafasi yao katika kukomesha rushwa. Hata hivyo, katika msitari wa 20 na 21 tunaona wala rushwa wakitumia mbinu ya pesa ili kuwarubuni wananchi na wapinga rushwa ili wawaachwe waendelee na vitendo vya rushwa. Katika mistari hiyo kunasemwa, "*Nikasema sijali, nikatoa pesa mfukoni*', "*Nikanunua mayai, kilichofuata watu hawakai*', "*Mayai*". Hapa imetumika kuonesha namna wala rushwa walivyo na njia nyingi za kurubuni ili waendelee na utaratibu wao wa kuchukuwa rushwa. Rushwa huwarubuni wadhibiti na wapingaji wa rushwa hali inayosababisha kuendelea kufanya vitendo vya rushwa. Hata hivyo, si wadhibiti wote wanaokubali kurubuniwa, wapo wenye msimamo na hufanya kazi yao kwa uaminifu na uadilifu.

Matabaka

Matabaka katika jamii ni dhamira ambayo imewasilishwa katika kazi mbalimbali za fasihi ikirejelea utabaka uliokuwepo katika kipindi cha Ukoloni na uliopo hivi sasa katika jamii. Utabaka hujitokeza pale kunapokuwa na kundi la watu wenye nacho na wasio nacho ambapo wenye nancho huwa ni bora na wasio nacho huwa ni watu wa chini. Watu wa tabaka la juu na wale wa tabaka la chini hushirikiana kwa pamoja katika kutimiza masuala mbalimbali ya kimaisha. Katika ubeti wa 2 msanii anaonesha kuwa siku ya Jumapili ndiyo siku maalumu kwa watu wenye ufahari

kwenda kutembelea maeneo mbalimbali ya starehe, hasa katika fukwe za bahari. Kauli hii inajibainisha katika mistari ya 22 mpaka 24 anaposema, "*Ilikuwa Jumapili*", "*Siku ya watu wenye ufahari"* na "*Kujirusha sehemu mbalimbali*". Misitari hii inathibitisha kuwa wapo watu wa tabaka la juu na la chini katika jamii. Suala la kuwepo kwa matabaka katika jamii ni kitu ambacho hakiepukiki, lakini mbaya ni ile kuwa na utofauti mkubwa sana wa hali ya maisha baina ya matabaka haya mawili. Kuwepo kwa matabaka ndiko kunakofanya maisha yaweze kuendelea kwani matabaka hayo yanahitajiana ili kukamilishana.

Katika jamii zipo baadhi ya kazi ambazo daima huwa hazifanywi na watu wa tabaka la juu, bali hufanywa na watu wa tabaka la chini. Mathalani, katika msitari wa 29 msanii anasema, "*Nikaomba embe sokoni*"", huu ni msimbo wa kimatukio ambao unaonesha kuwa mtu wa tabaka la chini anaweza kufanya kitu au vitu nyenye manufaa kwa watu wa tabaka la juu. Baada ya kupewa embe sokoni alikwenda nalo mpaka baharini na kuwakuta watu wa tabaka la juu wakiwa katika starehe zao. Haya yapo katika msitari wa 30 na kuendelea ambapo watu wa tabaka la juu walitamani na kuomba wapewe embe hilo. Hii inaonesha kuwa watu wa tabaka la juu huwategemea watu wa tabaka la chini katika kukamilisha mambo mbalimbali ya maisha yao kama ilivyo watu wa tabaka la chini huwategemea wale wa tabaka la juu katika kujikimu kimaisha. Msanii anasisitiza anaonesha namna mtu wa tabaka la chini lilivyo na mchango muhimu katika kusukuma mbele maisha ya mtu wa tabaka la juu.

Ukarimu

Ukarimu ni kitu muhimu sana katika kukamilisha maisha ya Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Hali hii imefanya duniani kote kuzifahamu jamii za Kiafrika kuwa ni za watu wenye ukarimu wa hali ya juu. Ukarimu ni hali ya kumuengaenga mgeni au mtu yeyote yule kwa huduma na kumfanya kufurahia kwa kujiona kuwa yeye ni mtu muhimu sana hata kufanyiwa ukarimu wa aina hiyo. Katika mataifa ya kibepari, suala la ukarimu huwa halizingatiwi sana kwa sababu kila mtu hujali maisha yake na ya familia yake tu. Hii ni kutokana na utamaduni wao ambao ni wa kibinafsi (Nyerere, 1962). Msanii katika wimbo wa '*Msiniseme*' ameiwasilisha dhamira ya ukarimu pale tunapoelezwa kuwa msanii alitaka kula, lakini hakuwa na pesa na aliamua kwenda sokoni kuomba embe. Alipatiwa embe hilo alikwenda nalo baharini. Msitari wa 29 ndio usemao, "*Nikaomba embe sokoni*," ikiwa na maana kuwa embe hilo lilitolewa bure bila ya kulipiwa. Katika hali ya kawaida si rahisi kwenda kwa mfanyabiashara na kumuomba kitu ambacho kinauzwa akupe bure bila malipo. Tukio hilo linaonesha utamaduni wa jamii ya Watanzania kukirimiana bila ya kujali hasara.

Katika mataifa ya Ulaya Magharibi na Marekani ni vigumu sana kuona ukarimu wa namna hii kwani kama mtu hana fedha ni vigumu mno kupata huduma yoyote ile.

Kila kitu ambacho mtu anakitaka ni lazima akipate kutokana na kufanya malipo. Utamaduni wa aina hii unaonekana pia katika baadhi ya nchi za Kiafrika na mfano mzuri ni Kenya ambapo hata kuulizia mahali fulani ni wapi unatakiwa ulipe fedha ili uelekezwe. Matumizi ya kauli kama "*Naomba nipe kitu fulani*" si rahisi kuyakuta katika nchi ya Kenya, bali katika nchi ya Tanzania ambako hata mtu akinunua kitu dukani anatumia neno naomba na huku amelipa fedha. Ukiwa nchini Kenya unatakiwa kusema nipe kitu fulani kwa sababu umekilipia hujapewa bure. Hii inaonesha kuwa bado ukarimu ni sifa kubwa kwa nchi ya Tanzania na hata wageni hufurahia sana nchi hii kutokana na ukarimu wa watu wake, hasa ikizingatiwa kuwa hii ni nchi yenye historia ya kijamaa tofauti na Kenya ambayo ina historia ya kibepari.

Umoja na Ushirikiano

Jamii za Kiafrika zinasifika sana kuwa kufanya mambo kwa ushirikiano katika masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kiutamaduni. Hili linaonekana bayana hata katika kipindi cha kupigania uhuru wa nchi za Afrika kutoka kwa Mkoloni nchi za Afrika ziliungana pamoja ili kuhakikisha kuwa kila nchi inapata uhuru wake na kujitegemea kama nchi (Nyerere, 1962). Nchi ya Tanzania ilikuwa ndio mahali maalumu kwa wapigania uhuru kukutana na kupanga mikakati ya namna ya kuhakikisha nchi zao zinapata uhuru. Nchi za Afrika ya Kusini, Msumbiji na Zimbabwe ni mfano wa nchi ambazo ziliitumia ardhi ya Tanzania kwa ajili ya kujifua ili kumuondoa Mkoloni huku serikali ya Tanzania ikishirikiana nazo bega kwa bega na kwa hali na mali. Ushirikiano wa aina hii umekwenda mbali mpaka kwenye matukio ya kijamii kama misiba na sherehe za harusi. Kunapokuwa na tukio la huzuni kama msiba au sherehe kama ndoa na harusi wanajamii husika hushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha jambo linalohusika linafanikiwa.

Katika wimbo wa '*Msiniseme*' msanii ameonesha aina hii ya ushirikiano kupitia ubeti wa kwanza ikiwa ni mistari ya 10 mpaka 16. Mistari hii inaonesha kuwa kulikuwa na shughuli mtaani; na alipokuwa akipita aliona watu wamekaa katika shughuli hiyo ndipo naye akaamua kwenda. Alifika wakati ambao ni wa chakula na moja kwa moja akaanza kula na hakuulizwa na mtu yeyote, isipokuwa pale alipoonekana kuwa anakula kwa fujo pasipo ustaarabu ndipo akafukuzwa. Msanii anasema "*Kulikuwa na pilau na wali*," "*Basi nami nikajiunga*," "*Pale pale kupiga mpunga*," "*Watu wakajipanga*," anaonesha kuwa hakuna mwanajamii aliyezuiliwa kushirikiana na wenzake katika jambo lolote lile zuri kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Mistari hii pia imetumika kwa lugha ya ishara ikitoa taswira kuwa kushirikiana katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya jamii ndio msingi mkubwa wa maendeleo.

Mapenzi

Mapenzi ni moja kati ya dhamira kuu katika nyimbo za Bongo Fleva kiasi kwamba inatajwa kuwa takribani asilimia 90 ya nyimbo hizo huwasilisha mapenzi (Devos, 2007 & Omari, 2009). Mapenzi yanayoelezwa katika nyimbo za Bongo Fleva ni yale ya kimahusiano ya mke na mume ambapo vijana hueleza namna wanavyowapenda au kupendwa na wenzi wao. Pia, huelezea visa na mikasa inayowakumba katika mapenzi. Hii ni hali ya kawaida kwa vijana kwa sababu wapo katika umri ambao unawaruhusu kuzungumzia masuala hayo. Msanii amewasilisha dhamira ya mapenzi kwa namna ambayo si rahisi kuonekana kwa jicho la haraka haraka. Katika ubeti wa pili, dhamira ya mapenzi inaonekana hasa katika msitari wa 28 mpaka 38. Katika mistari hii amechora picha inayoonesha kuwa alipita sokoni kuomba embe, kisha kwenda nalo baharini katika ufukwe maarufu wa matajiri.

Kinachosemwa hapa si embe la kawaida tunalolifahamu, bali ni msichana mrembo ambaye inavyoonekana alikwenda naye ufukweni na mara baada ya kufika huko matajiri walianza kumtamani. Msanii anasema, "*Napita na embe kiutani*", '*Nakula ili watamani*", "*Mate yaliwajaa midomoni*" na "*Basi wote wakaanza kuniomba*". Mistari hii inayoonesha kuwa msanii alikuwa na msichana mrembo aliwachanganya watu wenye ufahari huko ufukweni. Jambo hii linaonesha kuwa katika jamii mapenzi hayachagui wala kubagua kwani mtu wa chini anaweza kuwa na mahusiano na msichana mzuri zaidi kuliko hata watu wenye fedha. Hili linathibitika pale tunapoelezwa kuwa matajiri walianza kumeza mate mara baada ya kuliona embe. Msanii ametumia ufundi wa hali ya juu sana katika kujenga dhamira ya mapenzi kiasi kwamba mtu ambaye hajaiva kinadharia hawezi kuiona dhamira hii, badala yake ataishia kusema kuwa wimbo hauelezi mambo ya msingi.

Hitimisho

Wimbo '*Msiniseme*' umesheheni dhamira mbalimbali zinazohusu rushwa na ufisadi, matabaka, ukarimu, ushirikiano na mapenzi katika jamii. Makala hii imewasilisha dhamira hizi kama mchango ama sehemu katika kujibu hoja iliyoibuliwa katika Kongamano la Bongo Fleva lililofanyika mwaka 2010 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wasanii wengi walihoji kuwa wimbo huo ulipewa nafasi kubwa katika vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi, lakini hauelezi mambo ya msingi kwa manufaa mapana ya jamii na taifa kwa ujumla. Wasanii kadha wa kadha walisikika wakidai kuwa 'Mtu anasifia kula tu, lakini kila chombo cha habari unachofungua unasikia wimbo huo unapigwa kwa kweli hii si sawa?' Msingi mkubwa wa kauli hii unatokana na ukweli kuwa wahusika waliutazama na wanaendelea kuchunguza wimbo huu kijuujuu tu bila kuzama na kutafakari kwa makini yanayosemwa ndani yake. Kutokana na uchambuzi wetu huu, tunaamini kuwa wachambuzi na wahakiki wengi zaidi wa fasihi ya Kiswahili watatoa mchango wao katika kuuchambua wimbo huu kwa undani kifani na kimaudhui.

Marejeleo

Askew, K. (2002). *Perfoming the Nation: Swahili Music and Cultural Polities in Tanzania*. Chicago: The Universsity of Chicago Press.

Barthes, R. (1994). *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Berg, B. L. (2009). *Qualitative Research Methods for the Social Sciences (7 Ed*). Boston MA: Pearson Education, Inc.

Chandler, D. (1992). *Semiotics: The Basics*. London: Routledge Press.

Clack, M. K. (2013). "The Struggle for Hip Hop Authenticity and Against Commercialization in Tanzania.' *The Journal of Pan African Studies Vol. 6, No. 3, pp. 15-32*.

Devos, J. (2007). *The Evolution of Hip Hop Culture*. Torhont: Katho Department.

Mark, G. (1995). *Postmodern Semiotics: Material Culture and the Forms of Postmodern Life.* Oxford: Basil Blackwell.

Njogu, K., na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Nyerere, J. K. (1962). *Ujamaa: The Basis of African Socialism*. Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Omari, S. (2009). 'Tanzanian Hip Hop Poetry as Popular Literature.' Unpublished Phd. Thesis University of Dar es Salaam.

Omari, S. (2011). 'Call Me Top in Dar es Salaam: The Role of Pseudonyms in Bongo Fleva Music'. *Swahili Forum 18 pp. 69-86*.

Perullo, A., & John, F. (2003). 'Language Ideologies, Choices and Practices in Eastern Africa Hip Hop." *Global Pop, Local Language, pp. 19-51*.

Umberto, E. (1976). *A Theory of Semiotics.* Bloomington: Indiana University Press.

Saussure, Ferdinand de. (1966). *A Course in General Linguistics* (W. Baskin, Trans.). New York: McGraw-Hill.

Solomon, J. (1988). *The Signs of Our Times: The Secret Meanings of Everyday Life.* New York: Harper & Row.

Suriano, M. (2006). *Hip Hop and Bongo Flavor Music in Contemporary Tanzania: Youth Experience s, Agency, Aspirations and Contradictions*. Gineva: UN.

Suriano, M. (2007). 'Mimi ni Msanii, Kioo cha Jamii: Urban Youth and Culture in Tanzania as Seen through Bongo Flavor and Hip Hop'. *Swahil Forum 14 pp. 207-223*.

Marriage and Domestic Violence in Tanzania: A Case of Moravian Christians in Mbeya City

Ngetelile Kajabila Makula
Teofilo Kisanji University.
makulangetelile1@gmail.com

Elia Shabani Mligo
Department of Theology,
Teofilo Kisanji University, Mbeya.
eshamm2015@gmail.com

Abstract
This article grapples with the question of violence in households in Tanzania. It examines the influence of domestic violence in Christian marriages. How do people in Christian households interpret the experiences of violence? A qualitative study was conducted in Mbeya City among Christians (pastors and lay) of the Movarian Church in Tanzania. It used interviews to determine the various experiences of violence in Christian marriages. The cultural explanation of violence was used as a theoretical perspective to interpret the obtained data. Findings indicate that most Moravian Christians at Mbeya City experience various forms of violence in their Christian households. This situation poses a serious challenge to the Church, the Moravian church in particular, in the way it handles the delicate institution of marriage for its vigor. The article suggests that the Moravian Church and other churches, as servants of Jesus Christ, have a considerable obligation to eradicate violence in Christian marriages.

Keywords: Christian Marriages, Economic Violence, Sexual Violence, the Moravian Church, Physical Violence and Psychological Violence.

Introduction

The words of Pil (2014) are important to begin with as we clarify the concepts of marriage and domestic violence. Pil says: "Today, fashion is manipulating society, and it is one of the most influential factors in modern civilization. We can understand this word modern or fashionable as all which is different than before, everything which is beyond old, as something new, unusual and different, in one word – contemporary." There are various definitions of marriage that reflect the contemporary life of people in Africa and the world at large. One such definitions conceives of marriage as a legally or formally recognized union between two people as partners in personal relationship. Marriage is the process by which one male and

one female make their relationship public, official and permanent. Özyiğit1 (2017) highlights what marriage really implies in contemporary time in the following statement:

> Marriage, which includes the coupling of two people possessing different interests, desires and needs, is a special association given shape by social rules and laws and significantly affects individuals' development and self-realizations. Functions such as meeting the need for love and being loved, meeting both individuals' biological, social, psychological and motivational needs, bringing new generations to world, gaining a place in society, the feelings of being safe and protected, the sense of cooperation, being confident about the future, feeling proud of each other and healthy functioning of sexual life, make marriage universal and significant for societies. Although its dimensions and contents have changed during human history, the institutions of family and marriage have maintained their universality and are still the core unit of societies." (Ogoma, 2014: 94).

Therefore, according to these two understandings, marriage is the joining of two people, a man and a woman in a bond that lasts until death; however, divorce can be allowed to cut off the bod to some non-Christian forms of marriages for some reasons like infidelity and a threat to kill one partner.

Marriage forms the initial founders of households where domestic violence is experienced. In this article, domestic violence is defined as any physical, psychological, sexual or economic harm to an intimate partner—husband, wife, child or any other member of the household. We will mainly focus on violence between husband and wife within households. Empirical studies indicate that sexual, physical, psychological and economic violence are prevalent in Sub-Saharan Africa (Kilonzo, et al., 2010). While most studies on violence in Tanzania have concentrated on the magnitude and factors associated with violence (Kazaura, Ezekiel & Chitama, 2016), the prevalence and risk factors (Stockl, Watts & Mbwambo, 2010), the way the church responds to domestic violence (Fumbo, 2013) and the relationship between women's employment status and domestic violence (Kinyodo & Joseph, 2020), there is hardly a study conducted to determine the experiences of violence in Christian marriages. The major problem in the study area is that most people encounter violence in Christian marriages but hardly report them to relevant authorities for steps to be taken against perpetrators. Therefore, the objective of this study was to determine how Christians experience domestic violence in Christian marriages.

Methodological and Theoretical Perspectives

As stated in the last sentence of the above paragraph, this study was set to determine the perceptions of domestic violence in Christian setting among Moravian Christians (pastors and lay) of Mbeya City area with a qualitative study. Qualitative studies fall under the interpretative paradigm where the researcher and the researched informants interact intimately with greater subjectivity, uses a small sample with detailed probing of issues (Corbetta, 2003). The article draws from interviews collected among the Moravian Christians at Mbeya City between March and May 2020 analyzed qualitatively to obtain themes from what they said. A sample of 10 Christians in Christian marriages (3 pastors and 7 lay) selected randomly was involved in the study taking into consideration of their genders. Informants participated freely in the study and interviews were conducted face-to-face at their consent after being informed about the objectives, issues of anonymity and confidentiality of information provided (Israel & Hay, 2006). For ethical purposes, the real names of informants are not mentioned in the presentation and discussion of data. Instead, letters A, B, C, D, E and F have been used for informants whose information have been used in this report on behalf of their real names.

The cultural causal theoretical perspectives as elaborated by Bowman (2003), have been used to interpret and discuss the presented data from informants. The cultural causal theoretical perspectives emphasize on the power of norms and traditions in particular situations as the main sources of domestic violence in various African households. They stick on conformity to cultural roles men and women and the elevation of men in society as an authoritative gender in African households. They further purport that some actions, for example, wife battering in African culture are made legitimate by culture itself through some issues implemented during the process of marriage such as the payment of bride price to the bride's relatives.

The payment of bride price makes it difficult for wives to leave abusive husbands because the payments sealed the contract between the families of the two couples (Bowman, 2003 & Apologun, 2020). In his words, Bowman states thus regarding the power of bride price that the payment of bride price to the wife's family at the time of their marriage makes it difficult for women to leave abusive husbands, unless their families of origin are willing to return the amount paid. The provision of bride price and the consideration of women as inferior to men, i.e., that women have no right to challenge the authority of their husbands, account for the rampant spread of violence between the marriage couples in marriages. Hence, by the use of these theoretical explanations to interpret and discuss the results of this research, the article argues that Christian marriages are equally vulnerable of domestic violence in various forms as those encountered in non-Christian marriages.

Experiences of Domestic Violence in Christian Marriages

Primarily, Christian marriage is conceived to be an honorable relationship with God's blessings, a covenant union between one man and one wife, expected to last in the whole life of the couples, whereby God is the contractor of the union in the presence of human witnesses. This matrimony has divine intention in it, that couples should stay joyfully, that they should support each other in their marital life and that they should not part in all circumstances whether of prosperity or of adversity. The couple should bear children and rear them according to God's wills. This section demonstrates that though most people in Mbeya City identify themselves as Christians, it is challenging for them to live in terms of teachings and practices of Christianity about non-violence in their marital relationships. It will be noted that there are various perceptions on violence and their causes in Christian marriages. We discuss some of such issues in the following paragraphs basing on the findings obtained during interviews with Moravian Christian informants.

Domestic Violence among Moravian Christian Marriages

There are many types of violence experienced by Moravian Christian marriages at Mbeya City according informants which include economic, physical, sexual and psychological violence. We briefly reflect on each one of them below:

Experience of Economic Violence

Economic violence is when the abuser has complete control over the victim's money and other economic resources or activities. Economic violence toward women occurs when a male abuser maintains control of the family finances, deciding without regard to women how the money is to be spent or saved, thereby reducing women to complete dependence for money to meet their personal needs (Fawole, 2008). It may involve putting women on strict allowance or forcing them to beg for money. This study discovered the existence of domestic economic violence among couples in Christian households. To justify the existence of economic violence in Christian marriages at Mbeya City, informant A (2020), a pastor, explains how she solved different problems relating to violence in Christian marriages. She reported that there was one Christian man who prohibited his wife from engaging into business in order to find her at home whenever he returned home. Informant A further said that, the Christian man could not allow his wife to do businesses because he believed that many business women did not respect their husbands. So, he thought that if his wife started getting money, she would start disrespecting him.

Informant B (2020) stated that she was prohibited by her husband to provide church's offering such as tithing and other offerings by the reason that he, as a husband, offers it and was enough because he was the head of the family. However, because that woman had a business, she provided God's offering from her business

